# Nipashe

Jumamosi Machi 18, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581253

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11


SUPA JACKPOT

TZS.1,090,583,531

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Shangwe** zatawala Mchungaji Kimaro kurudi Kijitonyama

UKURASA 3

# Samia: Uagizaji sukari, mafuta kufikia mwisho

UK. 2





Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Rulenge, Ngara, Severine Niwemuguzi, akiongoza maombi kwenye kaburi la aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, baada ya ibada maalumu ya kuadhimisha miaka miwili ya kifo chake. Ibada hiyo ilifanyika katika kanisa la Mt. Yohana Maria Muzeyi, Parikoa ya Mlimani, Chato, mkoani Geita jana. Wengine ni Mjane wa Magufuli, Janeth Magufuli, viongozi waandamizi wa serikali na wanafamilia. **Habari Uk. 3. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### RC YATANGAZA RASMI MACHI 17 KUMBUKUMBU YA KIFO CHA MAGUFULI

KANISA Katoliki Jimbo la Rulenge Ngara, limetangaza rasmi kuadhimisha kila mwaka, Machi 17 ambayo ni siku aliyofariki dunia aliyekuwa...

UKURASA WA 4

### KAMPUNI MPYA TEKSI MTANDAONI YATINGA

KAMPUNI ya SUKA ambayo inatoa huduma ya teksi mtandaoni imezinduliwa jijini Dar es Salaam na imeelezwa ...

UKURASA WA 5

### MGONJWA AFARIKI DUNIA KATIKA AJALI AKIWA KWENYE AMBULANCE

MGONJWA aliyekuwa akikimbizwa na gari la kubeba wagonjwa (ambulance) kwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) akitokea Morogoro, amefariki dunia na abiria watano ...

## CWT yakwepa mtego mahakama uchaguzi viongozi

UKURASA 2

## Mwalimu Mkuu mbaroni madai ya kifo mwanafunzi

UK.4


MICHEZO SIMBA SC KATIKA DAKIKA 90 HATARI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Irene John (wa tatu kushoto), akikabidhi mfuko mbadala kwa mmoja wa wageni waliotembelea banda la NEMC katika maonyesho ya kimataifa ya kilimo na mazingira nchini Qatar mapema wiki hii na kupewa elimu jinsi Tanzania ilivyofanikiwa kutokomeza matumizi ya mifuko ya plastiki. Wengine (kushoto) ni maofisa wa baraza hilo. **PICHA: NEMC**

# Samia: Uagizaji sukari, mafuta kufikia mwisho

**Na Halfani Chusi**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan amesema serikali imejipanga kuziba pengo la uagizaji nje ya nchi bidhaa zikiwamo mafuta ya kula na sukari pamoja na kutatua vikwazo vinavyoikabili sekta ya kilimo ili kumnufaisha moja kwa moja mkulima.

Samia aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa Jukwaa la Mfumo wa Chakula ambalo mkutano wake unatarajiwa kufanyika nchini kwa siku nne kuanzia Septemba 5, mwaka huu.

Uzinduzi huo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Tuzo ya Chakula Afrika, Waziri Mkuu Kasimu Majaliwa, Rais wa Zanzibar, Hussein Mwinyi, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, mawaziri na naibu mawaziri.

Alisema Tanzania imejitosheleza kwa chakula lakini ziko baadhi ya bidhaa hulazimika kuziagiza nje ya nchi na kwamba pengo hilo kwa sasa linatafutiwa ufumbuzi .

"Tuna mpango wa kufufua mashamba yote ya ndani na kulima kisasa zaidi kwenye mafuta ya kula. Sukari pengo letu ni tani 30,000. Kuna viwanda vinajengwa ambavyo vitakamilika mwakani. Kukamilika kwake kutapunguza pengo hili na tutafanikiwa kuzalisha sukari itakayotosha kwa matumizi yetu.

"Hadi kufikia mwaka 2030, tutafikia lengo la kuifanya sekta ya kilimo ichangie asilimia 30 kwenye pato la taifa na kulisha nchi jirani na bara la Afrika," alisema.

Pia alisema lengo lingine ni kuifanya Tanzania kuwa ghala la chakula Afrika na duniani kwa kuongeza tija katika uzalishaji kwa kuhakikisha wakulima wanapata mbolea na viuatilifu kwa wakati.

Rais alisema serikali itahakikisha vijana wanakuwa kipaumbele cha uwekezaji na kuwekeza kwenye utafiti, kufungua masoko mapya ya kimataifa pamoja na kujenga miundombinu imara na kuweka mazingira jumuishi sekta binafsi.

"Kwenye mnyororo wa thamani, wadau wa kilimo zaidi ya 30,000 watapata nafasi ya kujadiliana kuhusu kilimo hatua hii itaongeza uwezo kuzalisha chakula kupitia mpango wetu tuliouanzisha wa BBT (Be Better Tomorrow).

"Mikakati iliyowekwa kwenye kilimo tangu nchi ipate uhuru, imefanya nchi kujitegemea kwa chakula kile kinachozalishwa ndani ya nchi na wakulima wenyewe," alisema.

Rais Samia alitaja mafanikio mbalimbali yaliyopatikana hadi sasa kuwa ni pamoja na kuanzishwa kwa taasisi za utafiti, kuundwa kwa bodi za usimamizi mazao na mbegu, korido ya kilimo kusini mwa Tanzania, kuwapo kwa mazingira wezeshi kwa sekta binafsi yenye mnyororo wa thamani.

"Kwa upande wa kilimo cha mazao tumeanza kutenga maeneo ya kilimo kwa vijana na tarehe 20 (Jumatatu) nitakwenda kuzindua mpango Dodoma," alisema.

**KUONGEZA AJIRA**

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi alisema uwekezaji kwenye sekta ya kilimo utasaidia kupunguza tatizo la ajira nchini.

"Kuna vijana wengi nchini waliomaliza vyuo na wako mtaani, njia pekee ya kumaliza tatizo la ajira ni sekta ya kilimo, ninakushukuru Rais Samia, kwa wazo zuri la kuinua kilimo.

"Sisi kule Zanzibar watu wengi wamejiajiri kwenye eneo la uvuvi na ukulima wa mwani. Kwa hiyo tutakuwa tayari kuja kuwaonyesha namna shughuli hizo zinavyofanyika ili kuhamasisha watu wapende kilimo," alisema.

Rais mstaafu Kikwete alisema uzinduzi wa mifumo ya bei ya chakula Afrika ni mafanikio makubwa katika kutatua changamoto barani humo.

"Nina uhakika kwamba suluhu za chakula Afrika zinaweza kufanywa kutoka kwenye kongamano hili na Tanzania inaweza kuchukua nafasi muhimu katika kufanya kazi hiyo," alisema.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Mapinduzi ya Kijani barani Afrika (AGRA) ambaye ni Waziri Mkuu wa zamani wa Ethiopia, Hailemariam Desalegn, alisema miaka miwili iliyopita imeonyesha haja ya Afrika kubadilisha mifumo yake ya kilimo.

Rais wa AGRA, Dk. Agnes Kalibata, alisema taasisi hiyo inaamini nguvu ya Tanzania katika kulisha Afrika huku akibainisha kuwa ina uwezo wa kubeba mipango hiyo.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alisema Tanzania inatamani kujilisha na kulisha nchi zingine huku mipango mbalimbali ikiwekwa ili kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa na kuongeza kuwa serikali iko tayari kushirikiana na sekta binafsi katika kufanikisha hilo.

## CWT yakwepa kihunzi cha mahakama

**Na Oscar Assenga,** TANGA

CHAMA cha Walimu nchini (CWT), kimeruka kihunzi cha mahakama, baada ya kufanya mkutano mkuu wa dharura wa uchaguzi huku kikiacha nafasi za waliofungua kesi mahakamani.

Katika uchaguzi huo, CWT imejaza nafasi za Makamu wa Rais na Naibu Katibu Mkuu, huku kikikwepa kujaza nafasi za Mweka Hazina na Katibu Mkuu zilizozuiwa na mahakama.

Jana, CWT ilifanya mkutano huo jijini Tanga, huku kikitii amri ya kutozigusa nafasi hizo mbili ili kuepuka mkono wa sheria.

Akifungua mkutano huo, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, aliipongeza CWT kwa kutii katazo hilo la mahakama.

Kindamba alisema kufanyika kwa mkutano wa dharura na kuepuka kutovunja amri ya mahakama ni jambo jema ambalo linaonyesha ukomavu wao katika kutii sheria zilizowekwa.

"Kwa kweli niwapongeze kwa kutii katazo lililowekwa na mahakama ambalo limeweka zuio la nafasi hizo mbili za Mweka Hazina na Katibu Mkuu. Mmelithibitishia taifa kuwa mna ukomavu na kuna uimara CWT, chama imara na ngangari. Nawapongeza kwa ukomavu huo endeleeni hivyo hivyo kuwa walinzi wa watoto na wakufunzi wetu," alisema.

Awali, Rais wa CWT, Leah Ulaya, alisema chama hicho kinafuata sheria na taratibu zote za nchi kwa kuwa kinatambua kwamba walimu ni tegemeo la nchi, hivyo ni kundi ambalo linahitaji kuonyesha njia ya kuigwa katika kutii sheria za nchi.

"Ninaimani kwamba wajumbe wa uchaguzi watakuwa watulivu wataheshimu taratibu kwa Lengo la kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa utulivu na amani ili tuweze kupata viongozi wetu," alisema.

**AMRI YA MAHAKAMA**

Juzi, Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi Dodoma ilizuia mkutano huo baada ya kufunguliwa kwa kesi ya msingi kupinga kufutwa uanachama kwa waliokuwa viongozi wa chama hicho.

Viongozi hao ni aliyekuwa Katibu Mkuu, Deus Seif na Mtunza Hazina, Abubakar Allawi, ambao Desemba, mwaka jana, mkutano mkuu wa chama hicho uliazimia kuwavua uanachama huku wakiwa wanasubiri uamuzi wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kuhusu rufani ya kesi ya jinai.

Zuio la mkutano huo lilitolewa na Jaji Gerson Mdemu baada ya Seif na Allawi kuwasilisha maombi ya kuzuia uchaguzi wa nafasi hizo.

Akizungumza nje ya mahakama baada ya uamuzi huo, wakili upande wa waleta maombi, Nashon Nkungu, alidai uamuzi huo unatoa nafasi ya kusikilizwa kwa kesi ya msingi ya waleta maombi ya kuiomba Mahakama Kuu kutoa tafsiri ya mkutano mkuu wa nusu muhula wa CWT kuwajadili na kuwafuta uanachama wakati wakiwa na kesi mahakamani.

"Sababu iliyofanya waombe zuio la mahakama na kupewa ni uwapo wa kesi ya kujadili uhalali wa wao kuondolewa kama wanachama na kuondolewa kwenye nafasi za uongozi walizokuwa wakizitumikia," alisema.

Mkutano mkuu huo wa nusu muhula, uliazimia kuwafuta uanachama Seif na Allawi kutokana na kuhukumiwa kifungo cha miezi sita jela na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, baada ya kupatikana na hatia ya kutumia vibaya madaraka kwa kuchepusha Sh. milioni 13.9 ambazo ni mali ya CWT, hivyo kukosa sifa ya kuwa viongozi na wanachama.

Hata hivyo, wakati mkutano huo ukiazimia hayo, watuhumiwa hao walikuwa wamekata rufani wakisubiri hukumu kutoka Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam.

Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam ilitoa uamuzi kuhusu rufani hiyo ambayo Seif na mwenzake walishinda baada ya ushahidi uliotolewa kutowatia hatiani.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (watatu kushoto), akikata utepe kuzindua rasmi Chama cha Kampuni za Gesi ya Kupikia Tanzania (LPGA), jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni viongozi wa chama hicho, akiwamo Mwenyekiti Benoit Araman (wa tatu kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shangwe zatawala Mchungaji Kimaro kurejea Kijitonyama

**Na Mary Geofrey**

MCHUNGAJI wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Usharika wa Kijitonyama, Dk. Eliona Kimaro, jana alipokewa kwa shangwe usharikani hapo baada ya kumaliza likizo ya siku 60 aliyokuwa amepewa na uongozi wa juu wa kanisa hilo Dayosisi ya Mashariki na Pwani.

Mchungaji Kimaro jana alishiriki ibada ya masifu ya asubuhi (Morning Glory) baada ya kuwa l ikizo aliyopewa kuanzia Januari 16, mwaka huu. Awali, aliambiwa baada ya kumaliza likizo hiyo, anatakiwa kuripoti makao makuu ya dayosisi, Luther House, Dar es Salaam, ili kupangiwa majukumu mengine.

Akisalimia waumini wa ibada hiyo, Mchungaji Kimaro alimshukuru Askofu wa KKKT Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, kwa msamaha aliompatia wa kurejea katika usharika huo.

"Nimshukuru Baba Askofu kwa huruma na utashi wake kunirudisha tena kwenye usharika huu kwa sababu mimi ni mchungaji mwenye nadhiri za kichungaji. Nimeapa kutumwa na kuhudumu popote pale ambapo kanisa litaona nafaa kutumwa," alisema huku akishangiliwa na waumini hao.

"Kwa hiyo mimi si mali ya Kijitonyama mimi ni mali ya dayosisi na ingeweza kunituma mahali popote pale nami nikatii lakini bado nimerudishwa hapa kutumikia tena.

"Nawakumbusha tu kuwa kwa utaratibu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, mchungaji anaweza kutumwa mahali popote kwa hiyo naweza kuwa hapa au mahali popote pale na ningepokea kwa unyenyekevu," alisema.

Kabla ya kurejea kazini jana Mchungaji Kimaro, alitangaziwa msamaha wa adhabu ya likizo yake ya siku 60 na Askofu Malasusa akiwa katika Usharika wa Kinyerezi katika ibada ya shukrani iliyofanyika Februari 19, mwaka huu.

Akiwa ibadani hapo, Mchungaji Kimaro alitaja sababu ya kupewa adhabu hiyo kuwa ni kusifia vijana wa dini ya Kiislamu kuwa wana nidhamu ya kazi tofauti na vijana wa Kikristo.

Alikumbushia kuwa Novemba 13, mwaka jana, akiwa kwenye ibada ya mavuno katika usharika huo, aliongoza ibada na kuhubiri, kuwaombea wanafunzi wa kidato cha nne na vijana wasio na ajira.

"Mwishoni nilisukumwa kuwaombea wale vijana wasiyo na ajira na nilisisitiza suala la nidhamu 'Seif Discipline' na 'life Discipline' (nidhamu ya maisha) na katika kusisitiza, nilitoa mfano wa vijana wa usharika wangu wa Kijitonyama na wale wa dhehebu lingine, labda nitamke wazi wale wa Kiislamu.

"Baada ya hapo yale maneno 'yaliklipiwa' huko duniani na watu nisio wajua na kutengenezwa 'klipu' (video fupi) ambayo ilikuwa inaonyesha ulinganifu kati ya vijana wa kiislam na wakristo katika suala la uaminifu hasa vijana . Jambo hilo limeleta mtafaruku mkubwa ndani ya jamii na sintofahamu, wapo waliopekea 'Positive' na waliopokea 'negative' (hasi)," alisema Kimaro.

Mchungaji Kimaro alisema amepokea uamuzi wa Askofu Malasusa kama mchungaji mwenye kiapo na nadhiri ya daima za uchungaji, kutii maelekezo ya Askofu.

Naye Askofu Malasusa alitangaza kwa niaba ya washarika Mchungaji Kimaro, amesamehewa na aendelee, kutafakari na kukaa karibu na Mungu ili shetani asiwaondoe katika mstari.

Bila kutaja Mchungaji Kimaro kurejea lini kazini, waumini na wafuasi wa mchungaji huyo waliendelea kujiuliza maana ya msamaha huo hadi hapo jana aliporejea rasmi kuendelea na kazi.

Akiwa ibadani hapo Kimaro alitangaza jana jioni kwenye ibada ya masifu ya jioni angeendesha maombi ya toba na kuanzia Jumatatu ya wiki ijayo ataongoza ibada ya asubuhi na jioni kwa somo la kipindi cha kwaresma.

Itakumbukwa kuwa Februari 18, mwaka huu waumini na wafuasi wa Mchungaji huyo, walichanga zaidi ya Sh. milioni 10 kupitia kundi la WhatsApp na kubandika bango lenye picha yake eneo la Morocco wilayani Kinondoni.

Bango hilo ambalo hadi sasa lipo na picha yake lina maandishi yanayosomeka 'But The Greatest Of This Love' 1 Cor. 13: 13 na kichwa cha habari kikubwa kinachosema 'Let There Be Light' ikiwa na maana 'Na iwe Nuru', na ujumbe unaosema, 'Washarika na waumini wa Kijitonyama tunakupenda'.

Kusimamishwa kwa Mchungaji Kimaro, kulianza kufahamika, usiku wa Januari 16, kupitia video iliyokuwa ikisambaa kumwonyesha akiwaaga waumini wa ibada ya masifu ya jioni kuwa amepewa likizo ya siku 60 baada ya kuitwa katika ofisi ya msaidizi wa askofu na kufanya kikao na mkuu wa jimbo.

Katika video hiyo, Mchungaji Kimaro alitangaza kumaliza likizo yake Machi 17, mwaka huu, na baada ya likizo atatakiwa kuripoti Makao Makuu ya Dayosisi na si usharikani hapo tena, huku akiacha sintofahamu kwa waumini.

# Kanisa latangaza rasmi Machi 17 kumbukumbu ya kifo cha Magufuli

**Na Daniel Limbe,** Chato

KANISA Katoliki Jimbo la Rulenge Ngara, limetangaza rasmi kuadhimisha kila mwaka, Machi 17 ambayo ni siku aliyofariki dunia aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli.

Magufuli alifariki dunia Machi 17, 2021 wakati akipatiwa matibabu ya moyo katika Hospitali ya Emilio Mzena, Dar es Salaam, hali ambayo ilitikisa nchi na kuibua simanzi kwa wananchi.

Hali hiyo ilitokana na ukweli kwamba ilikuwa mara ya kwanza kwa taifa kushuhudia kifo cha Rais akiwa madarakani tangu kupatikana kwa uhuru wa Tanganyika mwaka 1961.

Ikiwa imetimia miaka miwili tangu kifo cha Dk. Magufuli, jana Kanisa Katoliki Jimbo la Rulenge Ngara, lilitangaza rasmi kuitambua na kuiadhimisha kila mwaka Machi 17 ikiwa ni kumwombea toba kwa Mwenyezi Mungu na kutambua mchango wake mkubwa kwa kanisa na jamii kwa ujumla.

Askofu wa Jimbo la Rulenge Ngara, Severine Niwemugizi, alisema Kanisa Katoliki jimbo hilo limeipitisha rasmi siku hiyo ambayo itaanza kuadhimishwa kila mwaka na kwamba waumini wa kikatoliki wanapaswa kuitambua kwa kumwombea heri Hayati Magufuli.

Askofu Niwemugizi alikuwa kwenye ibada ya misa takatifu ya kumwombea toba kwa Mungu, iliyofanyika jana kwenye Kanisa Katoliki Parokia ya Mlimani Rubambangwe, Chato, takribani mita 100 kutoka nyumbani kwao Hayati Magufuli. "Siku hii sasa ni rasmi kuiadhimisha kila mwaka. Mimi nitakuja hapa kila Machi 17 hata kama nitakuta waamini wawili. Hata kama nikiwa pekee yangu nitasali maana popote alipo askofu na kanisa liko hapo," alisema.

Askofu Niwemugizi alitumia fursa hiyo kumwombea Hayati Magufuli msamaha kwa yeyote aliyemkwaza enzi za uhai wake na kwamba huenda aliwakosea baadhi ya watu kwa kuwa naye alikuwa binadamu kama wengine.

Akizungumza kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Inocent Bashungwa, mbali na kushukuru kwa utumishi mwema wa Hayati Magufuli, amesema serikali itaendelea kuenzi mambo yote mazuri aliyotamani watanzania kuyapata.

"Ni miaka miwili imepita tangu tumempoteza aliyekuwa Rais wetu wa awamu ya tano, Hayati Dk. Magufuli. Ni ukweli usiopingika kuwa atakumbukwa sana na serikali na jamii kutokana na maono na alama zake za kimaendeleo alizozifanya kwa Watanzania," alisema Bashungwa.

Mjane wa kiongozi huyo, Mama Janeth Magufuli, aliwashukuru Watanzania kwa kuendelea kumwombea mema Hayati Magufuli sambamba na kulishukuru Kanisa Katoliki kwa kuendelea kumuenzi.

## HABARI KITAIFA

# Kampuni mpya teksi mtandaoni yatinga nchini

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya SUKA ambayo inatoa huduma ya teksi mtandaoni imezinduliwa jijini Dar es Salaam na imeelezwa kujibu changamoto za madereva na kutoa huduma bora kwa abiria.

Uzinduzi huo ulifanyika jana maeneo ya Posta jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Godfrey Daniel, alisema SUKA ni mfumo unaounganisha madereva na abiria kwa njia ya mtandao na teknolojia zingine.

"Katika lugha ya Kiswahili neno "Usukani" ni kifaa cha kuongozea chombo cha usafiri kama gari, piki piki, meli, ndege na kadhalika. Sasa kutokana na neno hilo, kukazaliwa au kuibuka neno lingine lisilo rasmi "SUKA" ikiwa ni mshika usukani au anayesuka njia yaani dereva," alisema.

Daniel alisema tangu awali kuanzia kwenye wazo na katika shughuli zote za ujenzi na ukamilisho wa mfumo wa SUKA, lengo limekuwa kuboresha na kujaribu kupunguza kama si kuondoa kero na changamoto anazopata dereva wa mtandao.

Alisema watayarishaji wa SUKA wanaamini kuwa ikiwa dereva atakuwa mwenye furaha na mafanikio kwenye kazi yake, hata viwango vya huduma yake vitakuwa bora zaidi na hivyo kuboresha huduma kwa mteja wake ambaye ni abiria.

"Baada ya utafiti tulioufanya, tuligundua na kutafuta suluhisho la changamoto ambazo dereva amekuwa akikumbana nazo ikiwemo makato ya juu, upatikanaji wa chenji, kutoheshimika katika kazi, kutokuwa na uhakika wa ajira mtandaoni kutokana na wenye mifumo kuizima au kumfungia dereva ama mabadiliko ya bei na mengineyo bila taarifa," alisema.

Kwa mujibu wa Daniel, SUKA ni mfumo unaofanya kazi na pia kutumika kwenye simu janja za Android na Apple na kwamba kama ilivyo mifumo ya namna hiyo, kuna App kwa ajili ya dereva na pia ya abiria.

"Tunajua kuwa madereva wako tayari na wamekuwa wakifanya shughuli zao kama kawaida na kupitia mifumo mbali mbali iliyopo. Dhumuni la kuleta SUKA na kinachotutofautisha na mifumo mingine ni kuwa sisi dereva ndiyo mteja wetu wa kwanza hivyo tumezingatia na tutaendelea kuboresha na kushirikiana na madereva walio na nia na utayari," alisema.

Alitaja vigezo vya kujiunga na mfumo wa SUKA na kuanza kutoa au kutumia huduma za usafiri kuwa kama ifuatavyo. Dereva wa SUKA anahitajika kuwa na leseni ya udereva halali iliyohai, Bima ya chombo husika iliyo hai, cheti cha LATRA (mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini) kilicho hai, simu janja na namba iliyosajiliwa.

"Abiria anapaswa kupakua app ya SUKA (ya blue kwa abiria) toka google play (android) au app store (iphone) tovuti yetu ya sukaride.com," alisema.

# Mwalimu Mkuu mbaroni kwa madai kifo cha mwanafunzi

**Na Vitus Audax,** ILEMELA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza, linamshikilia Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Mwinuko iliyopo Kata ya Kitangiri wilayani Ilemela, Mwalu Steven, kwa madai ya kutoa adhabu kwa wanafunzi 30 na mmoja akifariki dunia baada ya kuzungumza lugha ya Kiswahili tofauti na utaratibu wa shule.

Mwanafunzi aliyefariki dunia ni wa Glory Faustine (14) wa kidato cha kwanza huku Emmanuel Liatu (13) akivunjika mguu, baada ya kudondokewa na jiwe wakati wakitekeleza adhabu ya Mwalimu Mkuu ya kuchimba changarawe. Adhabu hiyo ilitolewa jana shuleni hapo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilbroad Mutafungwa, alisema wanamshikilia mwalimu mkuu huyo pamoja na mwalimu wa zamu, ambaye jina lake hakulitaja.

Alisema wanamshikilia mwalimu wa zamu kwa kuwa ndiye mwenye jukumu la kujua ratiba zote za wiki ikiwa ni pamoja na adhabu zinazotolewa na usalama wa wanafunzi wanaozitekeleza.

Kamanda Mutafungwa alisema kutokana na kifo cha mwanafunzi huyo, shule hiyo imefungwa kwa muda ili kuzuia taharuki ambayo imejitokeza na kuwataka wananchi kuwa watulivu wakati taratibu za kisheria zikiendelea kufanyika dhidi ya wahusika waliosababisha jambo hilo.

Alisema tukio hilo lilitokea siku hiyo majira ya saa 3:00 asubuhi wakati wanafunzi wakichimba changarawe na ghafla waliangukiwa na jiwe lililosababisha kifo na kujeruhi mwanafunzi mmoja. Kutokana na tukio hilo, wananchi wa maeneo hayo waliandamana ili kupata mwafaka na kuitaka serikali kuondoa adhabu kali dhidi ya wanafunzi. Mwanafunzi Jackline Jovin, ambaye ni miongoni mwa wanafunzi waliokuwa wakitekeleza adhabu hiyo, aliiambia Nipashe kwamba wakati wanaendelea na kazi hiyo waliona mawe madogo yakidondoka kwenye shimo walilokuwa wakichimba kwa ajili ya kupata changarawe.

"Tulitoka shimoni, mwenzetu alikataa kutoka akidai atatoka pindi atakapomaliza. Wakati tunatoka ndipo jiwe likaporomoka na kumwangukia kichwani Glory na jiwe hilo lilimkandamiza mguu Emmanuel wakati akitoka," alisimulia.

Getrude Michael, mzazi wa moja ya mtoto aliyekuwa akishiriki katika adhabu hiyo, alisema shule hiyo imekuwa ikitoa adhabu kali zinazopita uwezo wa wanafunzi na kuiomba serikali kuweka utaratibu mzuri wa utoaji adhabu kwa wanafunzi ili kuondoa matukio yanayosababisha madhara dhidi yao. "Hii sio mara ya kwanza kwa shule hii kutoa adhabu kali. Zimekuwa zikitolewa adhabu kubwa ikiwa ni pamoja na kubebeshwa matofali, kuchimba na kuhamisha vifusi na kuwaathiri kisaikolojia wanafunzi," alisema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kitangiri, Reuben John, alisema kutokana na jiografia ya mtaa huo wenye miamba mikubwa, hivi karibuni walifariki dunia watu baada ya kuangukiwa na mwamba wakati wakiendelea na shughuli za uchimbaji wa mawe. Alisema ajali za namna hiyo mpaka sasa katika mtaa huo zimeshatokea nne.

Muda mfupi baada ya tukio hilo, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji walifika na kuchukua mwili wa mwanafunzi huyo pamoja majeruhi na kuwapeleka katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Sekou Toure.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MWANZA | SAMSON JOSEPH KASHEKU | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 43118 LR MWANZA KIWANJA NAMBA 1535, KITALU 'A' NORTH BUSWELU ,KWA JINA LA JOSEPH LWIZA KASHEKU. 2.NYUMBA YENYE HATI NA. 52751 LR MWANZA KIWANJA NA. 973/1, KITALU 'B' NYEGEZI KWA JINA LA SAMSON JOSEPH KASHEKU 3.NYUMBA YENYE HATI NA. 52750LR MWANZA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA. 971/1, KITALU 'B' NYEGEZI KWA JINA LA JOSEPH LWIZA KASHEKU 4. NYUMBA YENYE HATI NA. 50140 LR MWANZA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA. 164, KITALU ' J' NORTH BUSWELU KWA JINA LA ZACHARIA MABULA KISUMO | 1.JOSEPH LWIZA KASHEKU 2.SAMSON JOSEPH KASHEKU 3.JOSEPH LWIZA KASHEKU 4.ZACHARIA MABULA KISUMO | 1.NORTH BUSWELU -MWANZA 2.NYEGEZI MWANZA 3.NYEGEZI MWANZA 4.NORTH BUSWELU-MWANZA | 12/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | MPOKI BROWN MWAIPASI | NYUMBA | MPOKI BROWN MWAIPASI | KILUVYA | 6/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | ROGIMWA AGRO COMPANY LIMITED | KIWANJA CHENYE HATI NAMBA 083KYL/1204 | SANGA ROGGERS GIDION MWAMENGO NA ANNA DANIEL | ITETE KYELA MBEYA | 5/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | UYACODE VICOBA PROGRAM | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI KNDO 29299-KND/MBR/MWZ/10/2 | UYACODE VICOBA PROGRAM HQ | MAKUBURI UBUNGO | 20/03/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KARIAKOO | RAMADHANI KITWANA IBRAHIM | NYUMBA | MARIAM KITWANA IBRAHIM | TABATA LIWITI | 5/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | THOMAS REMI MARKUS | NYUMBA | THOMAS REMI MARKUS | TABATA KINYEREZI | 6/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | PAULINA SAMSON PAULO | NYUMBA | SHUKURU HAMISI MADENGE | KIMBANGULILE-CHARAMBE | 12/04/2023 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | DADI SALUM HAMRI | NYUMBA | DADI SALUM HAMRI | KICHANGANI-KISARAWE II | 13/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | EDSON MAKALA DAUDI | NYUMBA | EDSON MAKALA DAUDI | KIROMO-BAGAMOYO | 06/04/2023 SAA 4:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | ARIEL JOHN MNGEREJA | NYUMBA | ARIEL JOHN MNGEREJA | ZINGIZIWA | 06/04/2023 SAA 4:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | HAMISI MESHACK NGINYANYI | NYUMBA | HAMISI MESHACK NGINYANYI | TABATA-LIWITI | 12/04/2023 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | AMANI OMARI NOMBWANI | NYUMBA | AMANI OMARI NOMBWANI | KIGOGO KISARAWE II -KIGAMBONI | 13/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | MINIHAJI HUSSENI MSHALE | NYUMBA | MINIHAJI HUSSENI MSHALE | GONGOLAMBOTO ULONGONI | 14/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | SHARIFA SAIDI HAMISI | NYUMBA | SHARIFA SAIDI HAMISI | PUGU BOMBANI, ILALA | 14/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.

2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.

3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0715868000/0714939933/0718038313/0787129539/076599900**

4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

# Serikali yapata dawa kampuni za bima kushindwa kulipa fidia

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru, ameipongeza Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Bima Tanzania (TIRA) na Benki ya CRDB kwa kutekeleza mchakato wa uanzishwaji wa Akaunti ya Dhamana ya Bima (Trust Account), akitaja suluhisho kwa tatizo la kampuni za bima kushindwa kuwalipa wateja wake.

Mafuru alipongeza hatua hiyo juzi wakati wa uzinduzi wa mafunzo ya utekelezaji wa akaunti hiyo kwa Wakurugenzi Watendaji na maofisa wakuu wa fedha wa kampuni za bima nchini yaliyofanyika Makao Makuu ya CRDB, jijini Dar es Salaam.

Mafuru alisema uanzishwaji wa akaunti hiyo ni hatua nzuri ambayo itasaidia kuimarisha usimamizi wa sekta ya bima kuendana na matakwa ya kisheria na udhibiti yaliyowekwa na TIRA.

Akifafanua vikwazo vya awali, Mafuru alisema utaratibu uliokuwa unatumika mwanzoni katika usimamizi wa dhamana ya bima, haukuwa mzuri jambo ambalo lilichangia TIRA kushindwa kusimamia vizuri amana hizo pindi ziliporejeshwa kwa kampuni kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT) baada ya kuiva. Alisema kampuni nyingi za bima zilikuwa zinatumia fedha za amana ya akiba katika matumizi mengine, pasipo kupata idhini ya TIRA, hivyo kuingia katika changamoto ya ukwasi na wakati mwingine kushindwa kulipa fidia kwa wateja kutokana na fedha kuwekezwa katika miradi mingine.

Mafuru alibainisha kuwa uamuzi wa kufungua Akaunti ya Dhamana ya Bima katika benki za biashara ni mwarobaini wa changamoto hiyo kwa kuwa sasa TIRA itasimamia moja kwa moja fedha hizo za amana za akiba, jambo ambalo si tu litaimarisha usimamizi, bali pia kuboresha maendeleo ya sekta ya fedha.

"Niwapongeze CRDB kwa kuwa benki ya kwanza kuungana na TIRA katika uanzishwaji wa Akaunti ya Dhamana ya Akiba. Lakini nimevutiwa na namna ambavyo mmeona kuna umuhimu wa kuandaa mafunzo haya ambayo yanalenga kuwajengea uelewa kampuni za bima juu ya uendeshaji wa akaunti hiyo," alisema.

Mafuru alimtaka Kamishna wa TIRA kuhakikisha kampuni zote za bima zinafuata sheria kwa kuweka dhamana ya amana. Alisema kwa kufanya hivyo kutasaidia kuchochea mafanikio ya sekta ndogo ya bima kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Taifa wa Miaka 10 wa Kuendeleza Sekta ya Fedha nchini, 'Financial Sector Development Master Plan'.

Akizungumza katika warsha hiyo, Kamishna wa TIRA, Dk. Baghayo Saqware, alisema chimbuko la Akaunti hiyo ya Dhamana ya Bima ni Kanuni ya Bima ya Mwaka 2009 inayozitaka kampuni za bima kuweka amana za usalama angalau asilimia 50 ya kiwango cha chini cha mtaji halisi wa kampuni husika ya bima.

Dk. Saqware alisema mwaka jana mamlaka kwa kushirikiana na Chama cha Watoa Huduma za Bima (ATI), walikubaliana kuandaa Mwongozo wa Uwekazaji wa Usimamizi wa Ukwasi ambao pia ulielekeza uanzishwaji wa Akaunti ya Dhamana ya Akiba kupitia benki za biashara ili kuondokana na tatizo la changamoto ya kimtaji au kushindwa kulipa fidia za madai ya wateja wake.

"Mfumo unaokwenda kutumika katika akaunti hii mbali na kuboresha usimamizi, lakini pia ni rafiki na unaleta uwazi zaidi kwa wadau kwa maana ya kampuni za bima. Kampuni zitapata taarifa ya dhamana kwa wakati na kufanya uwekezaji kulingana na makubaliano na mamlaka," alisema Dk. Saqware. Akitoa taarifa za utendaji wa sekta ya bima, kamishna huyo alimjulisha Naibu Katibu Mkuu kuwa sekta hiyo imeendelea kukua kulinganisha na miaka iliyopita.

Alibaimisha kuwa mwaka jana mauzo ya bima yaliongezeka kwa asilimia 25 kufikia Sh. trilioni 1.146 kulinganisha na mauzo ya 2021, malengo ya mwaka huu ni kufikia Sh. trilioni 1.5.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid aliishukuru TIRA kwa kuipa fursa ya kushiriki katika uanzishwaji wa Akaunti ya Dhamana ya Bima.

Nsekela alipongeza uamuzi wa uanzishwaji wa akaunti hiyo na kusisitiza kuwa inachukua jukumu muhimu katika kukuza uwazi zaidi na uwajibikaji katika sekta ya bima na itakwenda kusaidia pia kujenga imani kwa wadau wa sekta hiyo.

# Mgonjwa afariki dunia katika ajali akiwa kwenye ambulance

Na Romana Mallya

MGONJWA aliyekuwa akikimbizwa na gari la kubeba wagonjwa (ambulance) kwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) akitokea Morogoro, amefariki dunia na abiria watano kujeruhiwa baada ya ajali kutokea eneo la Magomeni Mataa, mkoani Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Kamishna msaidizi (ACP) Mtatiro Kitinkwi, aliiambia Nipashe jana kuwa ajali hiyo ilitokea juzi majira ya asubuhi wakati' ambulance' ikimpeleka mgonjwa huyo Muhimbili ikiwa na watu sita, akiwamo dereva.

"Ajali hii ilitokea leo (juzi) Magomeni mataa na imehusisha ambulance T 730 BKD Landcruiser mali ya Hospitali ya Turiani iliyoko Morogoro ambayo imegongana na Coaster inayofanya safari zake Buza - Kawe yenye namba T 501 ATT.

"Ambulance ilikuwa kwenye mwendo wa haraka ikimuwahisha mgonjwa hospitali na Coaster ilikuwa kwenye haki kwa maana taa zilikuwa zinamruhusu kupita kuendelea na safari ya Buza alikokuwa anakwenda, matokeo yake ikatokea ajali," alisema.

Alisema ndani ya ambulance kulikuwa na watu sita ambao ni mgonjwa Iyan Kimei (53), aliyefariki dunia katika ajali hii.


MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TANGAZO KWA UMMA

**Utaratibu wa Kushughulikia Uingizaji wa Mizigo Nchini kwa Utaratibu wa Kuchangia Makasha "Cargo Consolidation & De-Consolidation"**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwakumbusha wananchi kwa ujumla na waagizaji wa mizigo kutoka nje ya nchi kupitia utaratibu wa kuchangia Makasha (Containers) ujulikanao kama "Cargo consolidation & De-consolidation" kwa kutumia mawakala wanaofanya shughuli hizi, juu ya umuhimu wa kuzingatia **Sheria, Kanuni na Taratibu** zinazosimamia utaratibu huo kama zilivyoainishwa kwenye sheria na kanuni; ***The Tanzania Shipping Agencies (Cargo Consolidator and De-Consolidator Regulation), G.N. No. 337 of 2018" hususani kifungu Na. 4 (1) (b), (c) na (m).***

Ni takwa la kisheria kwa mwagizaji wa mzigo anayetumia utaratibu huu kuhakikisha yafuatayo:-

**(i)** Wakala atakayemtumia kusafirisha mzigo wake ana leseni hai ya uendeshaji wa shughuli za "Cargo Consolidation & De-consolidation" inayotolewa na Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) kabla ya kuanza kufanya naye biashara,

**(ii)** Anatumia Wakala wa Forodha mwenye Leseni hai inayotolewa na TRA kupitia kwa Kamishna wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa,

**(iii)** Wakala wa Usafirishaji (Consolidator) anatoa nyaraka za kusafirisha mizigo kwa kila mchangiaji kwenye Kasha husika. Nyaraka hizi ambazo zinajulikana kama House Bill of Lading ndizo zitakazotumika kugomboa mizigo ya kila mchangiaji,

**(iv)** Anapata risiti sahihi ya huduma ya kusafirisha mizigo (EFD) kutoka kwa Wakala wa Usafirishaji pamoja na risiti ya huduma ya kugomboa mizigo bandarini ambayo inatolewa na Wakala wa Forodha.

Kwa upande wa Consolidators na De-Consolidators, wazingatie yafuatayo:-

**(i)** Kuhakikisha anafuata matakwa ya sheria tajwa hapo juu ambayo ni pamoja na kuwasilisha leseni yake ya uwakala wa usafirishaji (Consolidation & De-consolidation) kwa Kamishna wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa ili kukamilisha taratibu za kiforodha,

**(ii)** Kuhakikisha anakuwa na nyaraka kuu ya kusafirishia mizigo husika (Master Bill of Lading),

**(iii)** Anawapatia wamiliki wa mizigo nyaraka husika ili waweze kugomboa mizigo yao bila usumbufu baada ya kuwasili bandarini,

**(iv)** Kutimiza wajibu mwingine wowote kwa mujibu wa sheria za kodi nchini zikiwemo kuwasilisha ritani za VAT, ritani za kodi ya mapato na kutoa risiti sahihi za EFD,

**(v)** Kuwa ni kosa la kisheria kwa Consolidator au De-consolidator kugomboa na kulipia kodi mizigo ya watu wengine inayoingia nchini kwa kutumia jina la Consolidator au De-consolidator badala ya jina la mwenye mzigo.

Wafanyabiashara na Umma kwa ujumla unajulishwa juu ya kuzingatia tangazo hili ili kuisaidia TRA kutimiza wajibu wake ikiwa ni pamoja na kutunza taarifa sahihi za walipakodi nchini. Katika hatua nyingine tutafanya ukaguzi maeneo ya biashara ikiwa ni muendelezo wa ukaguzi wa kawaida kufuatilia namna wafanyabiashara wanavyoingiza mizigo yao nchini pamoja na kuhakiki nyaraka husika.

***Utekelezaji wa maagizo yaliyoko kwenye tangazo hili unaanza mara moja kwa mizigo inayoagizwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.***

***Aidha kwa wale ambao mizigo yao ipo njiani, wanapewa siku tisini (90) kuanzia tarehe ya tangazo hili wakamilishe taratibu za ugomboaji ikijumuisha ulipaji wa kodi stahiki.***

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na:**
**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPA KODI**
**TRA MAKAO MAKUU**

217327202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga wakati ni huu kuweka historia CAF

**SIMBA** na Yanga zote za jijini, Dar es Salaam ndio klabu pekee za Tanzania zilizobakia katika mashindano ya kimataifa ambayo huandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Leo Simba inatarajia kuwakaribisha Horoya AC kutoka Guinea katika mechi ya Kundi C ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kesho watani zao, Yanga watawaalika US Monastir ya Tunisia kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba na Yanga zilianza vibaya michuano hiyo kwa kupoteza ugenini, lakini baadaye zikaamka na kuanza kuvuna pointi.

Vigogo hao wa soka nchini, leo na kesho wanahitaji kupata ushindi wa aina yoyote ili kujihakikishia kusonga mbele katika michuano hiyo inayofanyika kila mwaka hapa Afrika kabla ya kusubiri mechi za mwisho zilizobakia ambazo watacheza ugenini.

Simba itamalizia kibarua chake Morocco kwa kuwakabili Raja Casablanca wakati TP Mazembe ya mjini Lumbumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) itawakaribisha mabingwa na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga.

Katika kuhakikisha timu hizo zinafanya vyema mechi zake za hatua ya makundi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan alitangaza kununua kila goli litakalofungwa katika michuano hiyo kwa gharama ya Sh. milioni tano.

Lengo kubwa la Rais Samia ni kuchagiza timu hizo kupata ushindi na hatimaye kusonga mbele katika mashindano hayo makubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Ahadi ya kiongozi huyo mkuu wa nchi bado inaendelea kwa timu hizo kongwe, hivyo mbali na furaha wanayoitafuta ya kutinga hatua ya robo fainali, lakini Rais Samia amefanya hivyo kuhakikisha heshima ya Tanzania inaendelea kuwekwa kwa askari wake hao.

Hamasa au motisha hiyo, imekuwa na maana kubwa kwa sababu mbali na wachezaji kuvuna fedha hizo, Rais Samia ameonyesha kushiriki katika mchakato wa kupata matokeo chanya kuanzia kwenye hatua ya maandalizi.

Tunawakumbusha wachezaji na viongozi wa Simba na Yanga, kuendelea kupambana kusaka ushindi na kuweka rekodi mpya ya timu hizo mbili kutinga robo fainali kwa pamoja, ndani ya msimu mmoja.

Huu ni wakati muhimu wa kila mhusika kufanya na kutekeleza vyema majukumu yake wakati vigogo hao watakapokuwa wanapeperusha bendera ya Tanzania kwenye ardhi ya nyumbani, kwa kuhakikisha pointi tatu za leo na kesho hazichukuliwi na wageni.

Kauli mbiu maarufu iliyokuwa inatumiwa na Simba isemayo 'Kwa Mkapa Hatoki Mtu' inatakiwa idumishwe na timu zote mbili pamoja na 'Full Shangwe kwa Mkapa' iliyotambulishwa na Yanga, zote zitendewe haki kwa kutoruhusu wageni kuvuna pointi.

Tunajua katika soka la sasa timu inaweza kupata ushindi hata katika uwanja wa ugenini, lakini tunaziombea Simba na Yanga kutoruhusu hilo wakiwa hapa nyumbani.

Wafahamu kusonga mbele katika michuano hiyo, si kutawapatia zawadi za fedha kutoka CAF, lakini kutaendeleza hatua ya Tanzania Bara kutoa wawakilishi wanne katika mashindano hayo ya Afrika.

Matokeo ya ushindi katika mechi hizi mbili za nyumbani kutawapa raha mashabiki na wanachama wa soka nchini ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakiumizwa na klabu zetu kuwa wasindikizaji kwenye michuano hiyo ya kimataifa.

Kama ambavyo Rais wa Heshima wa Simba, Mohammed Dewji 'Mo' aliwahi kusema ndoto yake ni kuona siku moja Mnyama anatwaa ubingwa wa Afrika na Rais wa Yanga, Hersi Said, amekaririwa akisema timu yao itakuwa ya kwanza kuleta kombe la Afrika Tanzania, kauli hizo ziwe za kweli kwa kufanya kila linalowezekana kuileta furaha hiyo wakati huu ambao Rais Samia akiwa bega kwa bega na wanamichezo.

Kila la heri Wekundu wa Msimbazi, Kila la heri Yanga. Mungu ibariki Tanzania katika michuano ya Afrika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kongole TFF, TWFA kwa Ligi Bora ya Wanawake msimu huu

**WAKATI** Ligi Kuu ya Soka la Wanawake inaanza kuchezwa hapa nchini, ilionekana kabisa kuna timu zimejitenga kwa ubora, baadhi zikiwa na uwezo mkubwa huku nyingine zikionekana kabisa zinasindikiza kutokana na udhaifu.

Timu zilizoonekana kuwa na uwezo ni ile inayomilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), iitwayo JKT Queens.

Kutokana na ubora wake, iliweza kushinda taji la ligi hiyo mara mbili mfululizo tena bila kupoteza mechi, ikiwavua ubingwa Mlandizi Queens, ambao waliweka rekodi ya kuwa timu ya kwanza kutwaa ubingwa wa soka wanawake nchini katika msimu wa mwaka 2016/17 Baadaye kulianza kuwa na mwamko wa baadhi ya klabu hata za Ligi Kuu hususan kubwa za Simba na Yanga kuanzisha timu za wanawake.

Simba ilianzisha timu yake ya iliyoitwa Simba Queens na baadaye watani zao wa jadi, Yanga nao walianzisha ya kwao, inayoitwa Yanga Princess.

Mwanzoni hazikuonekana kuleta ushindani sana, lakini baadaye Simba ilianza kukusanya wachezaji bora kutoka Mlandizi Queens na JKT Queens kuunda kikosi bora ambacho kilitengeneza timu imara.

Ilichanganya na wachezaji wachache kutoka nje ya nchi kama Asha Djafar na Joelle Bukuru, wote raia wa Burundi ambao ni moja ya wachezaji wa kigeni wa mwanzo kabisa kwenye kikosi hicho.

Uwekezaji wa klabu ya Simba katika kikosi chao cha wanawake (Simba Queens), kiliifanya kuwa tishio, na mpaka sasa ni mabingwa mara tatu mfululizo wa ligi hiyo.

Utawala wa kikosi hicho kimekuwa chachu kwa wapinzani wao Yanga Princess nao kukitengeneza kikosi chao, ambapo msimu uliopita walianza kusajili wachezaji bora, wakiwamo kutoka nje ya Tanzania.

Msimu huu ndiyo kabisa, huenda ikawa ndiyo timu yenye wachezaji wengi wageni kuliko timu yoyote kwenye Ligi Kuu.

Siyo Yanga Princess tu, timu kama Fountain Gate Princess, Baobab Queens, Alliance Queens, The Tigers Queens siyo tu kama zimesajili baadhi ya wachezaji kutoka nje, lakini pia zina makocha wageni pia.

Nitoe pongezi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF) na Chama cha Mpira wa Miguu Wanawake Tanzania (TWFA) kwa kuweka mazingira rafiki kiasi soka la wanawake limeanza kuwa na ubora, hasa msimu huu wa ligi.

Kuruhusu klabu kusajili wachezaji wa kigeni kwa ajili ya kuleta chachu, pamoja na makocha wa kigeni kumesababisha ligi hiyo sasa kuwa ngumu na yenye ushindani kama Ligi Kuu Tanzania Bara.

Zamani timu zilikuwa zinafungana zaidi ya mabao 10 na hata ukiangalia uwanjani unaona kabisa utofauti kati ya timu moja na nyingine, lakini kwa sasa hili linaanza kufutika kuanzia msimu huu.

TFF na TWFA hawakuweka kanuni nyingi za kuwalinda wazawa, badala yake wameacha wageni walete chachu na kweli, imewafanya hata wachezaji wa Kitanzania kuwa na viwango vikubwa wakigombania namba na wenzao.

Hilo limesababisha ligi kuwa na upinzani, kiasi tumeona Simba Queens ikifungwa na JKT Queens mabao 2-1 katika mechi ya ufunguzi, Yanga Princess ikichapwa bao 1-0 dhidi ya Fountain Gate Princess na hata timu ya mwisho, Mkwawa Queens ikaing'ang'ania Yanga Princess na kutoka nayo suluhu hivi karibuni.

Mipango madhubuti ya kuendeleza na kupandisha kiwango cha Ligi Kuu ya Wanawake kwa ujumla, matunda yake yanaonekana mpaka kwenye msimamo wa ligi hiyo ambapo kwa mara ya kwanza timu zimekuwa zikifungana na kuachana kwa pointi chache, kuliko hata Ligi Kuu Tanzania Bara ya wanaume. Mpaka sasa Simba Queens na Fountain Gate zote zina pointi 26, zinatofautiana tu mabao ya kufunga, mabingwa watetezi wakiwa wanaongoza.

Tofauti na zamani ambapo timu bingwa ikuwa ikionekana tangu mwanzo, msimu huu timu moja kati ya nne zilizoko katika nafasi ya juu, inaweza kuwa bingwa kwa sababu hazijaachana sana pointi.

Hata kwenye orodha ya ufungaji bora wachezaji wamefungana, wanne wakiwa na mabao tisa kila mmoja, nao ni Donisia Minja wa JKT Queens, Cynthia Musungu wa Fountain Gate Princess, Opa Clement na Jentrix Shikangwa wote wa Simba Queens.

Musungu na Shikangwa ni Wakenya, Donisia na Opa ambaye amekwenda kucheza soka la kulipwa Uturuki ni Watanzania.

Kwangu mimi hii ndiyo Ligi Kuu bora zaidi ya wanawake kuwahi kutokea, na naamini TFF na TWFA wanaendelea kuweka mazingira rafiki, pamoja na kusaka wadhamini ili msimu ujao ubora zaidi uonekane kwa maslahi ya kukuza soka.



Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Prof. Shedrack Mwakalila akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mafanikio ya chuo hicho, kwa kipindi cha miaka miwili ya Awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, ambapo imefanikiwa kuanzisha miradi mbalimbali katika kampasi zake za Karume, Pemba. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Mwalimu Nyerere yageukia utafiti kutatua kero uchumi

**Na Romana Mallya**

CHUO cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), kimesema kulingana na taaluma za wahadhiri kilio nao, kimejipanga kutoishia kufundisha darasani pekee, bali kufanyia utafiti changamoto zikiwamo za kiuchumi na kuzitoa ili zisaidie kupata ufumbuzi wa matatizo.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Shadrack Mwakalila, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na wahariri kuhusu mafanikio ya miaka miwili katika kampasi zake za Kivukoni, Zanzibar na Pemba, tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani. "Tunataka utafiti unapofikia mwisho utolewe kwa idara au wizara husika badala ya kufungiwa kwenye makabati. Tunataka matokeo ya utafiti yaende kuleta suluhu ya nini kifanyike," alisema.

Kuhusu mafanikio ya chuo, Prof. Mwakalila alisema wamefanikiwa kuongeza wanataaluma wenye Shahada ya Uzamivu (Ph.D) kutoka 37 hadi 46. Alisema wamefanikiwa kutoka mafunzo ya uongozi na maadili kwa viongozi na watendaji kutoka taasisi mbalimbali na wanafunzi kwa zaidi ya watu 4,000.

"Tumefanikiwa kuongeza idadi ya walimu na wahadhiri wenye PhD kutoka 37 mwaka 2020 hadi kufikia 46 mwaka huu," alisema na kuongeza kuwa udahili wa wanafunzi umeongezeka kutoka 11,413 mwaka 2020/21 hadi kufikia 14,457 mwaka 2022/23.

Alisema katika Kampasi ya Kivukoni wameboresha miundombinu katika mabweni ya wanafunzi, madarasa na ofisi za wafanyakazi na kuweka umeme jua kwenye mabweni na barabara chuoni hapo.

Pia alisema wamekarabati nyumba za wafanyakazi na kanteeni na kuboresha mfumo wa majitaka.

"Tuna ujenzi wa maktaba unaoendelea hapa umefikia asilimia 30, ikikamilika itakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kujisomea kwa mara moja na kutakuwa na kumbi za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000," alisema.

Prof. Mwakalila alisema katika Kampasi ya Karume, kuna ujenzi wa mabweni unaendelea yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 1,536 kupitia fedha Sh. bilioni mbili zilizotolewa na serikali.

Katika Kampasi ya Pemba, Prof. Mwakalila alisema wanatarajia mwanzoni mwa mwezi ujao kujenga madarasa na jengo la utawala kwa Sh. bilioni 2.6 zilizotengwa.

"Tumehuisha Sera ya Uthibiti Ubora ili kuhakikisha kuwa, mafunzo tunayotoa yawe ni bora na yenye viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

"Mchakato wa kuandaa mitaala mipya na kuhuisha mitaala ya zamani umekamilika ili kuwa na mitaala inayozingatia mahitaji halisi ya kitaifa na kimataifa," alisema.

Kiongozi huyo alisema katika maboresho hayo somo la uongozi, maadili, na uzalendo limeingizwa katika mitaala yote ili kila mwanafunzi awe na ufahamu wa kutosha kuhusu uongozi, maadili na uzalendo.

Alisema chuo kimetenga bajeti kwa ajili ya kuwawezesha wahadhiri kufanya tafiti mbalimbali zenye maslahi chuoni na kwa taifa na tayari wahadhiri wamejengewa uwezo wa kuandika maandiko ya utafiti na machapisho.

Prof. Mwakalila alisema chuo kimewezesha wahadhiri 56 kwenda kwenye mafunzo kwa ngazi mbalimbali za masomo ikiwamo Shahada ya Uzamivu, Shahada ya Umahiri, Shahada ya Awali na Stashahada.

Alisema idadi ya watumishi imeongezeka baada ya kupata kibali cha ajira za wahadhiri 86 na kufanya jumla ya watumishi wa kudumu kwa sasa kuwa ni 305.

Pia alisema chuo kimekuwa na bunifu zaidi ya 22 ambazo zimeshindanishwa kwenye maonesho mbalimbali, huku moja ikishika nafasi ya pili kitaifa katika mashindano ya maonesho ya Kitaifa ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) na nyingine nafasi ya nne kitaifa.

# Kamati yaundwa kupata suluhu migogoro ya wakulima, wafugaji

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SERIKALI ya Kijiji cha Kimambira, Mvomero mkoani Morogoro, imeunda kamati ya wafugaji na wakulima ili kuondoa migogoro na ugomvi baina yao ambayo husababisha uvunjifu wa amani licha ya kuwekwa sheria ndogo za kuwabana wafugaji kulinda vyema mifugo yao.

Kaimu Mwenyekiti wa Kijiji, Hassan Mbega, alisema hayo juzi kwenye shamba la mkulima aliyelishiwa mazao yake huku akibainisha kuwa migogoro baina ya wafugaji na wakulima ni tatizo linalosumbua kijiji na wilaya hiyo kwa miaka mingi na mpaka sasa bado hawajapata majibu kamili licha ya kuanza kuyadhibiti.

Mbega alisema kamati hiyo ina lengo la kujenga umoja wa kirafiki kwa kumfanya mfugaji kuelewa mipaka yake ya kuchungia na mkulima awe na haki ya kulima.

Alisema wataalamu wa sekta ya mifugo kutoka halmashauri ya wilaya, walishatembelea maeneo hayo na kutoa maelekezo ya sheria ndogo za halmashauri kwamba ng'ombe mmoja akiingia shambani kwa kila hatua anayokanyaga, analipishwa Sh. 15,000.

Mbega alisema kijiji hicho kina wakazi 1,200 ambao wengi wao ni wafugaji na wakulima na mara kwa mara wamekuwa wakipokea kesi kutoka kwa wakulima kuhusu wafugaji kuingiza mifugo katika mashamba yao.

Awali, wakulima wa kijiji hicho walisema wanaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuelimisha wafugaji kuchunga katika maeneo maalum waliyotenga ili kuepusha kero ya kuruhusu mifugo kula mazao mashambani na kuwasababishia hasara na uharibifu wa mali sambamba na kuwaingiza kwenye baa la njaa bila kutarajia.

Mmoja wa wakulima hao, Kasilima Kampuni, alisema akiwa mkulima wa miaka mingi katika kijiji hicho, amekuwa akikumbana na tatizo la wafugaji kulisha mifugo kwenye shamba lake lenye ukubwa wa ekari 12 na baadaye kushindwa kulipa.

"Kwa mwaka huu, hii ni mara ya nne wafugaji hawa wanaingiza mifugo kwenye shamba langu. Nimerudia tena kupanda lakini wameingiza tena mifugo na nikisema nao bado wanasumbua kwa kubadili wachungaji kwenye ng'ombe wa mtu mmoja anayejulikana kwa jina la Taiyei na wanakataa kulipa. Sasa sisi wakulima tufanyeje?" alihoji.

Alisema amekuwa akivuna magunia 13 hadi 14 kwa ekari hizo 12 kutokana na mifugo hiyo kula mazao shambani na kumfanya kutofikia malengo yake ya kilimo anayokusudia licha ya kupoteza fedha nyingi kwa ajili ya kununua pembejeo za kilimo, kuandaa shamba, mbegu, kupanda na palizi.

# Mkandarasi abanwa kususasua kwa mradi

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

SERIKALI imemwagiza mkandarasi wa ujenzi wa Kituo Jumuishi cha Taasisi za Kisheria za Serikali Mkoa wa Mwanza, SUMA JKT, kukamilisha ifikapo Oktoba 23, mwaka huu, ili wananchi waanze kupata huduma.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, wakati Kamati ya kudumu ya Bunge ya Utawala Bora, Katiba na Sheria ilipotembelea kituo hicho na kufanya ukaguzi.

Mradi huo wa miezi 18 unaogharimu Sh. bilioni 3.8 unatakiwa ukamilike Oktoba 23, mwaka huu, na hadi sasa umefikia asilimia 45 badala ya asilimia 55 kama ilivyotarajiwa.

"Serikali haidaiwi na haijachelewesha malipo kwani tuliwapa kazi hiyo tukifahamu mna uwezo wa kufanya kazi saa 24. Hatutegemei ucheleweshaji wowote na hatutaongeza muda. Hakikisheni mnakamilisha ifikapo Oktoba 23 ili wananchi waanze kupata huduma," alisema.

Mbunge wa Kishapu, Boniface Butondo, alionyesha wasiwasi huenda mkandarasi akashindwa kutekeleza mradi huo ndani ya miezi minane iliyobaki kwa kuwa walitegemea uwe umefikia asilimia 65 badala ya 45 sasa.

Mbunge wa Singida Kaskazini, Ramadhan Ighondo, alimtaka mkandarasi aongeze kasi ya utendaji nguvu kazi na muda afanye kazi usiku na mchana,asitegemee kuongezwa muda maana gharama zitaongezeka na anapopata changamoto ya malipo aiambie serikali pia ilipe kwa wakati mradi usikwame.

Aidha, Mbunge wa Viti Maalum Kundi la Wenye Walemavu, Khadija Kaaya 'Keisha', alisema matatizo ya mradi kuchelewa ni yale yale na yanajirudia, hivyo itafutwe tiba ili kazi zifanyike kwa ufasaha.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Utawala Bora, Katiba na Sheria, Florent Kyombo, alisema licha ya ucheleweshaji kidogo wa mradi, mambo yaliyochangia au kurudisha nyuma utekelezaji yafanyiwe kazi ili kuendana na kasi inayotakiwa na kuukamilisha.

"Tumeubariki mradi huu na tunauhitaji sana ili kuwapunguzia wananchi gharama na umbali wa kufuata huduma,mradi ni mzuri hivyo ongezeni kasi kama tulivyokubaliana ukamilike kwa muda uliopangwa," alisema.

Awali, akitoa taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa mradi huo, Kapteni Ferdinand Sira, alisema mradi huo una changamoto mbalimbali zilizochangia uchelewe kwa miezi miwili lakini wameandaa mpangokazi utakaoendana na muda wa kukamilika kwa mradi.

Kapteni Sira aliahidi kufanya kazi usiku na mchana kutekeleza mradi huo kwa weledi na juhudi ili ukamilike kwa wakati na ubora unaotakiwa na kuishukuru Kamati hiyo ya Bunge kuwatembelea kuona maendeleo ya mradi huo.




Mkurugenzi Mkuu wa Sotta Mining Ltd, Dk. Joas Kabete (kulia), akijadiliana jambo na Kamishna wa Tume ya Madini, Prof. Abdulkarim Mruma (katikati) na Mjumbe wa Kamati ya Maudhui ya Ndani anaeiwakilisha Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Ringo Ringo, wakati wa jukwaa la pili la ushirikishwaji wa watanzania kwenye sekta ya madini, jijini Arusha mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa: Fichueni wanaoharibu vyanzo vya maji

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa wito kwa wananchi kutunza na kuhifadhi mazingira na kuwafichua watu wanaohujumu mazingira na vyanzo vya maji.

Alisema hayo juzi wakati akizungumza na wadau mbalimbali wa sekta ya maji na mamia ya wananchi waliohudhuria uzinduzi wa mradi wa ujenzi wa Mfumo wa Usambazaji Maji kati ya Makongo na Mji wa Bagamoyo. Uzinduzi huo ulifanyika sambamba na uzinduzi wa Wiki ya Maji kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Tegeta A, Dar es Salaam.

Majaliwa alisema licha ya juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali za kuboresha miundombinu ya ukusanyaji na usambazaji wa maji, ni jukumu la kila Mtanzania kutunza vyanzo vya maji. "Tuna jukumu kubwa nalo ni la kutunza na kuhifadhi vyanzo vya maji na eneo hili tuna mgogoro mkubwa kwani vyanzo vyetu vya maji vinaharibiwa, ni wajibu wetu kutunza vyanzo hivi," alisema,

Waziri Mkuu alisema Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alishatoa mwongozo wa uhifadhi wa vyanzo vya maji na kila Mtanzania anapaswa kuzingatia hilo.

"Suala la uhifadhi ni muhimu sana, DAWASA isimamie suala hili kwa karibu na kutoa taarifa mapema, wakurugenzi wa Mabonde ya Maji nchini kama vile Ruvuma, Rufiji, Malagarasi na mabonde mengine yote hakikisheni mnafanya ukaguzi wa mara kwa mara ili vyanzo hivi visiharibiwe," aliagiza

Aidha, alisema wananchi wanawajibu wa kulinda vyanzo hivi na iwapo mtu ataonekana akiharibu kisima au chanzo kingine wachukue hatua ya kuzitaarifu mamlaka husika kwa kuwa huo ni sawa na uhujumu uchumi.

Akimkaribisha Waziri Mkuu kuzungumza na hadhara hiyo, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alimwagiza Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Kiula Kingu, ahakikishe wananchi wote walioomba maji wafungiwe mita ndani ya siku saba kama Mkataba wa Huduma kwa wateja unavyosema.

Kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji kwenye wizara yake, Waziri Aweso alisema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha nyingi kwenye wizara hiyo ambazo ni mahsusi kwa utekelezaji wa miradi ya maji.

"Mheshimiwa Rais kwa sasa ametoa asilimia 90 ya fedha za utekelezseeaji wa miradi ya maji, wakati awali utekelezaji ulikuwa ni kati ya asilimia 50 hadi 60 tu," alisema.

Alisema Serikali bado inafanya jitihada kubwa zaidi katika kuhakikisha kila maeneo yanapata maji hivyo kila mmoja anapaswa kulinda vyanzo vya maji.

# Mjadala ujenzi sanamu Mwalimu Nyerere waiva

**Na Halfani Chusi**

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Amina Shabani, amesema miongoni mwa hoja zitakazowasilishwa kwenye mkutano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), ni pamoja na ujenzi wa sanamu ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kwenye Makao Makuu ya Umoja wa Afrika (AU).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kauli hiyo aliitoa juzi, kwenye ufunguzi wa mkutano wa kamati ya kudumu makatibu wakuu wa SADC, unaofanyika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Alisema pamoja na kujadili kuhusu sanamu hilo, pia watakumbushia Tafsiri ya Nyaraka muhimu za SADC, kuwekwa katika lugha ya Kiswahili ambayo ni hatua muhimu ya utekelezaji wa matumizi ya lugha hiyo kwenye jumuiya.

Mengine ni Mpango wa kanda wa ununuzi wa pamoja wa bidhaa za afya unaoratibiwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na mkakati wa pamoja wa Kanda wa Kusimamia Sekta ya Mbolea.

Mwenyekiti wa mkutano huo ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Mtangamano wa Kikanda wa DRC, Balozi Songhu Kayumba, aliwasihi wajumbe kushiriki kikamilifu kwa kutoa maoni yatakayolenga kufanikisha utekelezaji wa agenda zitakazojadiliwa.

Alisema makatibu wakuu na wajumbe watajadili agenda mbalimbali ambazo ni pamoja na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa maamuzi ya wakuu wa nchi na serikali waliyotoa katika mikutano iliyopita.

# Kamati Bunge yapongeza programu ya KKK

**Na Munir Shemweta,** MERU

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii imepongeza Program ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK) inayotekelezwa na Halmashauri ya Meru katika shamba la Valeska lililokuwa linamilikiwa na Chama cha Ushirika cha Mkoa wa Arusha (ACU).

ACU ilishindwa kuendeleza shamba hilo na kusababisha kufutwa na Rais Mei 22, 2018 kwa mujibu wa kifungu namba 45 cha Sheria ya Ardhi na ufutwaji huo kusajiliwa Septemba 27, 2018.

Maelekezo ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusiana na eneo la shamba hilo ni vijiji vinavyozunguka shamba la Valeska ambavyo ni Kwaugoro, Maroroni na Valeska ni kutengewa ekari 500 kila kijiji kama mpango wa mgawanyo wa shamba ulivyopendekeza.

Akizungumza wakati wa ukaguzi utekelezaji mradi wa KKK kwenye shamba hilo juzi, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii Timotheo Mnzava, aliipongeza halmashauri ya Meru kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Alisema halmashauri hiyo ni ya mfano kati ya halmashauri mbalimbali nchini zilizokopeshwa fedha na wizara ya ardhi.

"Hapa niipongeze sana serikali na hasa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kazi anayoifanya ikiwamo kutoa fedha za kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Meru imekuwa mfano kwa kazi nzuri waliyoifanya," alisema.

Mbunge wa Makete, Festo Sanga, alitoa pongezi kwa halmashauri ya Meru kwa utekelezaji mzuri wa program hiyo na kueleza kuwa kilichofanyika ni moja ya vitu vikubwa vilivyofanywa na halmashauri nchini. Alisema halmashauri zingine nchini zina cha kujifunza kupitia mradi huo wa KKK na Meru ni kielelezo na mfano.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alisema Meru ni halmashauri ya kipekee kati ya halmashauri zilizopatiwa mkopo usio na riba na wizara yake na kufanikiwa kuurejesha mkopo huo kwa asilimia mia moja.

"Sisi kama serikali tunaichukulia halmashauri ya Meru kama halmashauri ya kipekee kwa kukopa na kurejesha mkopo kwa asilimia 100," alisema.

Dk. Mabula pia alimpongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Meru, Mwalimu Zainabu Makwinya, kwa kujali na kuihudumia vyema idara ya ardhi kwa kuipatia vifaa sambamba na kujali watumishi tofauti na halmashauri nyingi zinazoifanya idara ya ardhi kuwa kama mtoto yatima.

Halmashauri ya Meru ilipatiwa mkopo usio na riba wa program ya kupanga, kupima na kumilikisha (KKK) wa Sh. bilioni 1.655 kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi .

Hadi kufikia mwisho wa mradi, mkopo huo umesaidia halmashauri kulipa fidia, kupanga, kupima, kufungua baadhi ya miundombinu ya barabara na kumilikisha kama mwongozo wa mkopo ulivyotolewa.

Halmashauri ya Meru inatarajia kupata mapato kutokana na mradi wa KKK ya Sh. 8,466,795,725 na faida ya mradi baada ya kutoa gharama za mradi na gharama za viwanja vya fidia 418 yenye thamani ya Sh. 598,231,950 inatarajiwa kuwa Sh 6, 213,563,775.





# TANROADS, TARURA zapewa maagizo mazito

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAKALA wa Barabara Tanzania (Tanroads) na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) zimeagizwa kufikisha miundombinu ya barabara kwenye maeneo ya uwekezaji ili kuwavutia wawekezaji.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alitoa agizo hilo jana wakati wa kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Dodoma.

Senyamule alisema taasisi hizo zinapaswa kuhakikisha maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji yanajengewa miundombinu ya barabara ili kuwavutia wawekezaji.

Kadhalika, alisema TARURA na TANROADS zinatakiwa kuangalia uwezekano wa kuingia mkataba na sekta binafsi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo ili kufanikisha lengo la kuwavutia wawekezaji.

Alisema ucheleweshaji wa ujenzi wa barabara hizo unawafanya wawekezaji kukata tamaa ya kuwekeza huko kutokana na maeneo husika kufikika kwa shida.

Kwa mujibu wa Senyamule, wawekezaji wanakuwa na mitambo ya kuingiza kwa ajili ya kazi zao lakini wakikutana na miundombinu mibovu hawawezi kwenda huko.

Pia alisema serikali imewekeza fedha nyingi kwenye miundombinu ya Mkoa huo kwa kuanza ujenzi wa barabara za mzunguko na viwanja vya ndege.

Alisema mkoa huo umekuwa na miundombinu ya barabara zinazopitika muda wote hivyo wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza kwenye maeneo wilaya zote za Mkoa huo.

Aidha alisema alitaka taasisi hizo kutoa elimu kwa watumiaji wa barabara nchini ili kuepuka uharibifu wa miundombinu hiyo inayojengwa kwa gharama kubwa.

Awali, Mkuu wa Matengenezo TANROADS Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Salome Kabunda, alisema wanakusudia kujenga barabara ya Kongwa Mpwapwa kwa kiwango cha lami na zabuni ilitangazwa Machi 9, mwaka huu.

Mhandisi Kabunda aliyataja maeneo mengine ambayo ujenzi wa lami unaendelea kuwa ni Ntyuka iliyopo halmashauri ya Jiji la Dodoma hadi Mvumi Makulu wilaya ya Chamwino yenye urefu wa kilometa 25.

Barabara zingine kubwa ambazo wanakusudia kuzijenga kwa kiwango cha lami ni Kongwa Simanjiro ambayo itaunganisha Mkoa wa Dodoma,Manyara hadi Arusha.

Alisema katika mwaka wa fedha 2022/23 TANROADS imejenga na kukarabati baadhi ya barabara kwa kiwango cha lami.

# TANAPA yaja kivingine kuvutia watalii

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) limeweka mikakati ya kutoa elimu kwa umma ili kuongeza idadi ya watalii wa ndani na kufikia azma ya kupata watalii milioni tano kwa mwaka ifikapo 2025.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Hifadhi wa TANAPA wa Ofisi ya Kiunganishi Dodoma, Dk. Noelia Myonga, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za taasisi hiyo.

Alisema mikakati mbalimbali ambayo imewekwa na TANAPA, itasaidia kuongeza idadi ya watalii na kuongeza pato la taifa ikiwa ni pamoja na kupitia vivutio mbalimbali vilivyopo nchini.

"Sekta ya utalii nchini kwa hivi sasa inachangia pato la taifa kwa asilimia 17 na inachangia fedha za kigeni kwa asilimia 24," alisema.

Dk. Myonga alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na vivutio vingi ambavyo ni muhimu kuvitembelea lakini bado kuna tatizo la Watanzania wengi kutokuwa na mwamko wa kutembelea kwa kisingizio cha gharama kubwa.

Alisema Tanzania ina hifadhi 22 na kila moja ina mvuto wake na maajabu yake ambayo hayapatikani kwingineko duniani.

"Gharama si kisingizio kwani kwa watalii wa ndani kwa kuwa serikali imewapendelea wazawa ambao wanapenda kutembelea hifadhi zetu kwa kuweka gharama ya Sh. 11,800 kwa hifadhi kubwa na zile zingine ni Sh. 5,000 kiasi ambacho mtanzania anaweza kukimudu," alisema.

Alizitaja hifadhi hizo kuwa ni Arusha, Burigi -Chato, Gombe, Ibanda -Kyerwa, Katavi, Kigosi, Kilimanjaro, Kisiwa cha Rubondo, Kisiwa cha Saanane, Kitulo, Manyara, Mikumi, Mhale, Udzungwa, Mkomazi, Mto Ugala, Nyerere, Ruhaha, Rumanyika Karagwe, Saadani, Serengeti na Tarangire.

"Kila hifadhi imekuwa na mvuto wake tofauti kabisa. Mfano Hifadhi ya Manyara kuna Simba ambao wanapanda miti na ndege wazuri na waajabu na hifadhi ya Tarangire kuna tembo wengi na mibuyu mikubwa ambayo inavutia zaidi. Hifadhi ya Saadani kuna kasa wakubwa na wa kijani na vivutio vingi katika hifadhi mbalimbali," alisema Dk. Myonga.

Pamoja na kuhamasisha watu kutembelea hifadhi za taifa, alisema kuna haja ya Watanzania kujenga tabia ya kutembelea maeneo ya kihistoria ikiwamo michoro ya Kondoa Irangi, Kongwa maeneo ya wapigania uhuru.



Wahudumu wa afya wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, kitengo cha damu salama, wakiwahudumia watu walioamua kujitolea damu kwa ajili ya kuwasaidia wagonjwa, wakati wa maadhimisho ya miaka 70 ya Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kairuki aonya walimu ukiukwaji maadili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, amesema serikali haitasita kuwachukulia hatua kali walimu watakaobainika kwenda kinyume na maadili ya kazi.

Waziri Kairuki aliyasema hayo juzi wakati wa ufunguzi wa mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) uliofanyika jijini Dodoma uliokwenda sambamba na uzinduzi wa mfumo wa kielektroniki unaojulikana kama 'Teachers Service commission System (TSCMIS)'.

Alisema TSC ina wajibu wa kuwasimamia walimu ili watimize majukumu yao na kwamba walimu wanaitegemea tume hiyo, hivyo inapaswa kufanya kazi kwa weledi ili kuhakikisha walimu wanapata haki zao za msingi katika utendaji kazi wao wa kila siku. "Serikali haitakuwa tayari kuwavumilia walimu ambao wataenda kinyume cha maadili ya kazi. Nasisitiza TSC simamieni walimu kuhakikisha wanafanya kazi katika mazingira bora," alisema.

Kairuki pia aliagiza walimu kuhakikisha wanasimamia uendelezaji mradi wa kuboresha elimu ya sekondari nchini (SEQUIP) na ule wa Boost wa kuboresha elimu ya awali na msingi.

Alisema katika mradi wa SEQUIP serikali imeridhia kutumia Sh. trilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za sekondari 1026.

"Mradi wa BOOST serikali imeridhia kutumia Sh. trilioni 1.15 katika kipindi cha miaka mitano kwenye mwaka wa fedha 2022/23 zitumike kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa elimu na suala zima la miundombinu ikiwamo kuhakikisha mazingira ya ujifunzaji na kufundishia yanakuwa mazuri," alisema.

Alisema kupitia mradi wa BOOST, serikali itaendelea kuhakikisha walimu wanafundishwa kuzingatia ujuzi, lakini pia waendelee kuboresha mitaala na walimu ili kuendana na wakati ikiwemo kuhakikisha wanakuwa na uendelevu wa kuwapatia walimu mafunzo kazini.

Kuhusu mfumo wa TSCMIS, aliwataka TSC kutumia mfumo huo vizuri ili kurahisisha utatuzi wa kero mbalimbali za walimu, ikiwemo kupata taarifa sahihi za walimu.

Katibu wa TSC, Paulina Nkwama, aliishukuru serikali kutokana na kuajiri walimu,kupandisha madaraja walimu, vyeo, pamoja na kulipa madeni ya malimbikizo ya mishahara.





# SMZ yajivunia mabadiliko elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imesema imeingia katika mageuzi makubwa ya sekta hiyo ili elimu inayotolewa kwenda na wakati wa mahitaji yakiwamo sayansi na teknolojia.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa wizara hiyo, Lela Mohamed Mussa, wakati akifungua mkutano wa wadau wa elimu na kuwashirikisha washiriki wa maendeleo.

Alisema mabadiliko katika sekta ya elimu hayapaswi kuwekwa nyuma na yanatakiwa kwenda na wakati ili kuleta matokeo mazuri ikiwamo ufaulu wa wanafunzi.

Pia alisema katika uongozi wa sasa wa serikali ya Zanzibar chini ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, mabadiliko makubwa yamefanyika kwa lengo la kuleta mageuzi ya sekta ya elimu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Waziri huyo alisema miongoni mwa juhudi hizo ni serikali kuunda tume ya kuchunguza muundo wa elimu na mfumo wake, ambayo ripoti yake tayari imekabidhiwa serikali kuu na wadau wameanza kutoa maoni yao kwa ajili ya kuifanyia kazi.

Alizitaja juhudi zingine kuwa ni ujenzi wa shule za kisasa za ghorofa katika ngazi ya msingi na sekondari ambazo zimepunguza msongamano wa wanafunzi.

Kwa mujibu wa Waziri Lela, awali katika baadhi ya shule, wanafunzi darasa moja wanasoma zaidi ya 150 lakini sasa mikakati ni kuona darasa moja lina wanafunzi 45.

Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mwanakheir Adam Ameir, alisema wizara inatekeleza vipaumbele vya sekta hiyo ikiwamo kuimarisha elimu mjumuisho ambayo itawawezesha wanafunzi wa makundi tofauti wakiwamo wenye ulemavu kupata haki ya msingi ya elimu.

Mkurugenzi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), Michael Toto, alipongeza juhudi zinazochukuliwa na serikali katika sekta ya elimu.

# Siri wanawake kuwa nyuma kiuongozi zatajwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), Jamila Mahmoud, amesema kwa miaka mingi wanawake wameachwa nyuma katika maendeleo na hakuna usawa kati yao na wanaume Zanzibar.

Amesema mradi wa kumwezesha mwanamke kuingia katika nafasi za uongozi na kuwa na uongozi wa kidemokrasia, utasaidia kupaza sauti za wanawake na kujikomboa katika maendeleo, mradi huo unatekelezwa na ZAFELA.

Jamila aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wahamasishaji jamii wa nafasi ya mwanamke katika uongozi na waratibu wa kutetea haki za wanawake katika ngazi za shehia katika Chuo cha Elimu ya Watu wazima Rahaleo, mjini hapa.

Mkurugenzi huyo alisema ili kumpa fursa mwanamke kuwa kiongozi lazima awe na muda mwafaka, hivyo lazima kurahisishiwa majukumu ya kila siku na si kuachiwa kazi ya kuhudumia familia pekee.

"Mzigo wa mwanamke anaobebeshwa ndio unaomfanya ashindwe kuingia katika nafasi za uongozi kwa sababu asilimia 80 ya kazi za nyumbani, ikiwamo kuhudumia familia huachiwa mwanamke pekee na muda wake wote hupoteza huko," alisema.

Jamila alisema ili mwanamke awezeshwe katika kuitumia vizuri teknolojia lazima apunguziwe mzigo wa majukumu na kurahisishiwa huduma za kijamii kama vile hospitali na miundombinu ya maji safi na salama badala ya kwenda kutafuta maji masafa marefu. Ahlam Abdallah, mmoja wa wahamasishaji jamii katika masuala ya wanawake na uongozi, alisema wamefanya mikutano ya kijamii ndani ya shehia ili kuongeza ushajihishaji katika masuala ya wanawake, uongozi na demokrasia na kuwatumia wanawake vinara kama mfano wa kuigwa akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan ambaye kwa sasa anaongoza nchi vizuri.

Katika mikutano, alisema changamoto mbalimbali ziliibuliwa na kuonekana kuwa rushwa ni kikwazo kikubwa ambacho kinamkwamisha mwanamke katika uongozi.

"Pia changamoto nyingine ni hali duni ya kiuchumi kwa wanawake ambapo uongozi katika demokrasia unahitaji gharama" alisema.

Mratibu wa Miradi kutoka ZAFELA, Khamis Ali Rashid, alisema mradi huo umewafikia zaidi ya wananchi 5,000 kuwahamasisha kuwaunga mkono wanawake katika uongozi na demokrasia.

Alisema wananchi hao wamewafikia kwa kufanya mikutano katika shehia zao pamoja na kuwapatia mafunzo viongozi wa vyama vya kisiasa ili kuwaunga mkono wanawake katika uongozi.



Wavuvi wa kijiji cha Kizimkazi, Mkoa wa Kusini Unguja, wakikokota nyavu katika ufukwe wa bahari ya Hindi, kijijini hapo baada ya kurudi katika shughuli zao za uvuvi jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waandishi idhaa za Kiswahili kukutana Zanzibar

**Na Rahma Suleiman**

WAANDISHI wa habari wa lugha ya Kiswahili kutoka nchi saba duniani, wanakutana visiwani Zanzibar katika kongamano la Idhaa za Kiswahili Duniani na matumizi ya lugha hiyo linalotarajiwa kufanyika siku mbili.

Kongamano hilo litafunguliwa kesho na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, na kufungwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa katika ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdulwakil, Kikwajuni, Zanzibar.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA), Dk. Mwanahija Juma, alizitaja nchi hizo kuwa ni Uingereza, China, Uganda, Kenya, Burundi na wenyeji Tanzania.

Alisema katika kongamano hilo, mada mbalimbali zitawasilishwa ikiwamo changamoto za matumizi ya lugha katika idhaa za Kiswahili.

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema licha ya mada mbalimbali zitakazowasilishwa, pia kutakuwa na uwasilishwaji wa makala na mijadala na utoaji wa tuzo kwa waandishi wa habari.

Alisema pia kutakuwa na ziara ya kitalii kwa washiriki wa kongamano hilo kutembelea kisiwa cha Perison na kutakuwa na maonyesho ya vitabu na wajasiriamali.

Waziri Tabia alisema kutakuwa na tuzo za umahiri wa uandishi wa Kiswahili na kushajihisha matumizi fasaha na sanifu ya Kiswahili katika vyombo vya habari vya kitaifa na kimataifa.

"Aina ya tuzo hizo ni chombo bora cha habari cha runinga, radio, magazeti, mitandao ya kijamii na mwandishi bora anaetumia lugha sanifu na fasaha," alisema.



**HARMONIZE**
UKURASA 12

Nipashe BT BURU…
JUMAMOSI MACHI 18, 2023



# IGENI NA HILI

MJADALA mkali kwa sasa katika mitandao ya kijamii ni namna wasanii maarufu nchini Marekani, wanavyojizolea mabilioni ya pesa kwa ajili ya nyimbo wanazotakiwa kushirikishwa na wanamuziki wengine.

Suala hilo limeleta mitazamo tofauti, baadhi ya watu wanaunga mkono kwa kueleza ni moja ya vyanzo vya mapato, na wengine wanapinga kwa kueleza linadumaza sekta ya muziki kutokana na wasanii wengi wachanga kukosa fursa ya kuimba na wanamuziki wakubwa.

Kulingana na orodha mpya, inaonyesha mkongwe Marshall Bruce Mathers III, maarufu kama Eminem, anaongoza kwa dola milioni 3, sawa na shilingi bilioni saba.

Drake anashika nafasi ya pili kwa kutoza kiasi cha dola milioni 1, ambazo ni sawa na shilingi bil. 2.34.

Hata hivyo, wasanii wa bongo wanatakiwa kujifunza kwa wakongwe wawili Jay Z na Kanye West, ambao wao hawatozi chochote pale wanapotakiwa kufanya kolabo, bali wanaangalia heshima, mahusiano na ubora wa nyimbo.

Jay Z kweye mahojiano yake na Kevin Heart kwenye kipindi cha ‘Hart to Heart’ aliibua swali hilo na kusema yeye hatozi hata senti moja kwa msanii yeyote akitaka kumshirikisha bali anachozingatia ni heshima na msanii husika lakini pia aina ya wimbo anaoshirikishwa.

Wasanii maarufu wa hapa nchini wanatakiwa kujifunza hili, kwani licha ya rapa hawa kuwa maarufu na tena wenye pesa nyingi, lakini hawatozi pesa yeyote wanapotakiwa kushirikishwa, badala yake wanaangalia ubora wa nyimbo pekee.

Kuwatoza pesa wasanii wachanga wanaotaka kuinuka ni sawa na kuwaumiza kutokana na kutakiwa kutoa kiasi kikubwa cha pesa, pia kubebeshwa mzigo wa kutengeneza video na gharama za mavazi.

Pamoja na kulinda majina yao, lakini kuwe na utu pale wanapoombwa kufanya kolabo na msanii mchanga ikiwamo kuangalia ubora wa kazi yenyewe.

BASI SAWA

## Gigy Money kahemewa

MWANAMUZIKI mwenye kauli tata, Gigy Money, amesema kwa mara ya kwanza anaangalia jibu la



kumpa Zari, baada ya kumwambia zamani alikuwa mchafu.

Zari alimwandikia ujumbe Gigy Money, kupitia Instagram akimwambia wakati akiwa na mimba ya Tiffa alikuwa anaonekana mchafu na alionekana kama hakuwa na kawaida ya kuoga.

Lakini sasa amesafika muonekano wake, anaonekana kuwajibika zaidi na wa viwango.

Hata hivyo, Gigy Money amekuwa kimya tangu kutolewa kauli hiyo na ameeleza anatafakari nini cha kuongea kumwambia mama huyo wa watoto wawili wa Diamond Platnumz.

## Kadinda atupa dongo gizani



MBUNIFU wa mitindo na meneja wa mwigizaji, Martin Kadinda, amefunguka kwamba mrembo huyo aliwahi sana kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Diamond Platnumz.

Amesema Wema alikosa mapenzi kama alivyokuwa nayo kwa sasa kwa Whozu, na kwamba maisha yake yamejaa furaha na sio karaha kama ilivyokuwa kipindi cha nyuma.

Kadinda ameeleza kuwa yeye anachojua Wema na Whozu_ wanapendana na yeye anawatakia kila la kheri katika maisha yao ya mahaba.



## HARMONIZE MAISHA YAMEMFUNZA

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Harmonize, amempigia goti mama wa mtoto wake, akisema dunia imemfundisha kiasi ambacho kila siku anamkumbuka.

Mwimbaji huyo wa kibao 'Single Again' amemuahidi Mama mtoto wake maisha mazuri pamoja na kumnunulia nyumba na gari kwa kumzalia mtoto wa pekee, Zulekha.

Amesema maisha yao hawakuwa yatima bali wana mapenzi ya muda mrefu, lakini thamani aliyompa ya kuitwa baba ni wajibu wake wa kumbadilishia maisha kwa muda wa miezi miwili pekee.



## Wimbi la Joh Makini hilo!

RAPA mkali nchini, Joh Makini, amefanya mapinduzi ya muziki baada ya kuachia EP yake kupitia mtandao wa kijamii.

Joh Makini ametambulisha EP hiyo inayoitwa 'Wave' ambayo ndani yake kuna ngoma kali sita.

"Mwenyezi Mungu ni mwaminifu wimbi hili zito lenye mikwaju sita litatua rasmi duniani kote, ameandika Joh Makini katika ukurasa wake wa Instagram.

## INGEKUWA VIPI MWANA FA ANGETEULIWA BAKITA?

**Na Adam Fungamwango**

HIVI karibuni Tanzania iliweka historia mpya, ilipompata Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambaye ni mwanamuziki, akichaguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais Samia Suluhu Hassan.

Si mwingine ila ni Hamisi Mwinjuma, ambaye ni mwanamuziki, msanii mwimbaji wa muziki aina ya hip hop. Ni mmoja wa waanzilishi wa muziki wa bongo fleva ambao ulianza mwishoni mwa miaka ya 1990, na kuvuma zaidi mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Naibu Waziri huyo ambaye anajulikana kwa jina la kisanii Mwana FA, ni mmoja wa wasanii wakubwa nchini, ambao waliamua kujiingiza kwenye siasa, ambapo pia ni Mbunge wa Jimbo la Muheza.

Jina la Mwana FA limetokana na jina la Mwanafalsafa alilokuwa akilitumia mwanzo kabla ya kulifupisha.

Hakuitwa Mwanafalsafa kwa bahati mbaya, ukizisikiliza ngoma zake nyingi zina baadhi ya maneno ambayo mtu anapoyasikia inabidi akae na kutafakari.

Ngoma zake nyingi pamoja na kupendwa na mashabiki, lakini zikageuka kuwa misemo au misamiati hapa Bongo kila ukipita sehemu, hasa uswahilini.

Leo tunajikumbusha baadhi ya ngoma za Waziri Mwana FA, ambazo ziligeuka misamiati 'uswazi'.

**Ingekuwa Vipi**

Ngoma hii ilitoka mwanzoni mwa miaka ya 2000. Iliteka mashabiki wengi kutokana na maudhui ya ngoma yenyewe. Katika ngoma hii, Mwana FA alijaribu kueleza kuwa mara nyingi vitu vinakuwepo duniani kwa kutegemeana na ndiyo maana hiki kipo na hiki kipo. 'Angeimba nini Sister P kama asingekuwa Zay B, ingekuwa vipi miti, ingekuwa vipi Bongo mitumba isingehalalishwa, ingekuwa vipi ingekuwa ulipe buku tu kwa kila pumzi...?" ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye ngoma hiyo.

Jina la ngoma hiyo likageuka msemo hapa Bongo, kwani yeyote akitaka kuelezea jambo linalotegemeana na lingine basi atasema 'Ingekuwa Vipi.'

**Habari Ndiyo Hiyo**

Katika ngoma hii aliyomshirikisha AY, Mwana FA anaelezea vitu mbalimbali vinavyotokea ndani ya jamii, kuna vinavyowezekana na visivyowezekana na vya lazima na visivyo vya lazima. Anasema 'ndiyo maana kwenye kaburi hawaweki AC'. Ngoma hii ilitoka 2007 ilitamba kinoma na kutengeneza pia msemo kwa Wabongo.

Akikutana na mtu yeyote na kumweleza jambo ambalo anayeelezwa atashangaa, au ni jipya kwake, atamwambia 'habari ndiyo hiyo.'

Hata wale wenye tabia ya kusutana na kuzodoana, atakwenda kwa mgomvi wake na kumpasha, akishamaliza atamwambia tu 'habari ndiyo hiyo.'

**Unanitega?**

Hapa Mwana FA alikuwa akiwalenga akinadada wenye tabia ya kuvaa nguo zisizokuwa na staha, zile ambazo zinaonyesha asilimia kubwa ya maungo yao.

Baadhi wanavaa kwa sababu ya mazoea na malezi, wengine ni sababu ya kuwavutia wanaume.

'Mbona miguu iko wazi unanitega?, mbona kifua kiko wazi unanipenda?' Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye ngoma hiyo.

Hii ilitoka mwaka 2009 ilitokea kupendwa mno na mashabiki wa bongo fleva.

Mitaani sasa ikawa shida. Ngoma ikazaa msemo kwa akinakaka. Akipita demu tu akiwa na kanguo kafupi utasikia 'unanitega?'

**Bado Nipo Nipo**

Alitoa ngoma mwaka 2008 ambayo maudhui yake yaliacha wengi hoi na baadhi midomo wazi. Akasema kuwa yeye kuoa bado sana kwa sababu kila anapoona madhila wanayoyapata watu waliooa, kama vile kusalitiwa na vituko vingine vya ndani ya ndoa, hashawishiki kufanya hivyo.

Akasema anasubiri kwanza azeeke na siyo sasa, kwani bado yupo yupo tu.

FILAMU

## Shamba la Mnyonge halivunwi magugu

**Na Adam Fungamwango**

DHULUMA ni mbaya sana kwenye hii dunia. Ukitaka mambo yako yaende kombo, basi uwe na tabia ya kudhulumu watu. Ukitaka kuishi vema na kuwa na mwisho mzuri duniani, fanya kazi yako halali na ule kutokana na mali yake au kipato ulichonacho.

Wengi yamewakuta makubwa hapa duniani kutokana na tabia ya kutaka kudhulumu wenzao.

Halafu yeyote mwenye tabia hiyo pia hujiingiza kwenye mambo mengine mabaya zaidi kwa ajili ya kulinda dhuluma yake au kujikinga kwa sababu anajijua ana tabia mbaya.

Leo tuiangalie filamu inayoitwa 'Shamba la Mnyonge'. Ni filamu yenye mafunzo kwa jamii juu ya tabia mbaya ya udhulumati.

Imechezwa na kina Adili Add, Hawa Ramadhani, Said Ndibwa, Samuel Siwale, Hansdat, Said Mkima, Salim Katembo na wengine wengi.

Kijana Hassan aliyetokea Dar es Salaam, anawasili kwenye kijiji kimoja hapa nchini kutaka kununua shamba kwa ajili ya kilimo.

Anakutana na kijana mwingine anayemfahamu anaitwa Said na kumueleza azma yake hiyo.

Shamba linaloonekana kumvutia zaidi ni la Dati, mmoja wa wanakijiji wa hapo. Wanakwenda nyumbani kwake. Hata hivyo Dati anakataa kuuza shamba lake akidai kuwa ni la urithi kutoka kwa baba yake na ardhi kwenye maisha ya sasa ni mali, hivyo na yeye anawawekea watoto wake warithi.

Akamshauri kuwa kama anapenda eneo lile, basi aende kwenye shamba la jirani yake, huenda anaweza kumuuzia.

Said anampeleka Hassan kwa Mandevu. Huyu jamaa shamba lake linapakana na la Dati. Mandevu alivyosikia hivyo, tamaa ikamuingia. Akamwambia Hassan kuwa hata shamba la Dati ni lake, hivyo amuuzie yote mawili, lake na la Dati, kwani eneo lote ni la kwake.

Said akapinga, kwa sababu alijua si kweli. Kutokana na tukio hilo, Hassan akasitisha ununuzi kwanza, akisema suala hilo liwekwe sawa kabla ya kununua.

Uhasama ukaanza kati ya Mandevu na Dati. Mandevu akadai eneo lote lile ni la kwake. Kesi ikafika hadi Serikali ya Kijiji. Mwenyekiti wa Kijiji alisimamia haki. Akamwambia Mandevu hakuna hata hatua moja ya shamba la Dati ambalo atanyang'anywa.

Akitaka auze shamba lake tu. Hali hiyo ilimkasirisha Mandevu, akatangaza vita kwa wote waliosababisha washindwe kumdhulumu Dati shamba lake na kuliuza kwa Hassan.

Kumbe jamaa alikuwa mchawi. Akaanza kumpoteza Said kimazingara, halafu akaja Siwatu ambaye ni dada wa Dati. Akataka kummalizia na Dati kabisa. Akaenda nyumbani kwake kwa ajili ya kumfanyia kitu kibaya. Akanasa kimazingara.

Dati akamkuta hapo hapo amenasa. Akamwita mkewe aje amuone. Akaitwa na Mwenyekiti wa Kijiji. Ilikuwa ni aibu kubwa. Mwenyewe akakiri kuwa alikuwa na mpango wa kumuua Dati pamoja na familia yake ili apate shamba kirahisi, lakini ameshindwa na kuahidi kubadilika kuwa mtu mzuri kwa jamii, huku akiwarudisha Said na Siwatu ambao waliwaficha nyumbani kwake kimazingara.



# Davido hana kitu Instagram

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Davido amewashangaza mashabiki wake baada ya kufuta karibu posti zake zote za Instagram.

Msanii huyo, ambaye kurejea kwake kwenye mitandao ya kijamii kulitarajiwa na wengi, ameondoa picha yake ya wasifu na kufuta zaidi ya machapisho 4,000 ya matukio.

Davido aliacha picha tatu pekee, moja ya mtoto wake wa kiume, Ifeanyi Adeleke, aliyefariki Novemba 2022, mke wake, Chioma na moja ya onyesho lake kwenye Kombe la Dunia huko Qatar.



## Yaya apambana na jinamizi

ALIYEKUWA mshiriki wa Big Brother Titans, Yaya, amefunguka akisema kufukuzwa kwake na mpenzi wake, Marvin, ndani ya jumba hilo hakukuwa kitendo cha haki.

Mshiriki huyo amesema yeye na mwenzake kutoka Afrika Kusini, waliondolewa kimakosa.

"Hapana, sidhani kama ilikuwa sawa, nilifikiri bado tulikuwa na wiki mbili nzuri ndani ya nyumba kabla hatujafukuzwa." Amesema.

## Portable kawa bondia?

MWANAMUZIKI maarufu kutoka mtaani, Portable ameamua kujiandaa na mazoezi ya ndondi kwa lengo la kujilinda.

Msanii huyo amechukua hatua hiyo baada ya watu wasiojulikana kumshambulia kwa kipigo yeye na dada yake.

Katika video inayozunguka mitandaoni, inamuonyesha mwanamuziki huyo akifanya mazoezi ya ngumi bila kuvaa shati.





## Seyi kuolewa gani kimya kimya

MSANII wa muziki kutoka Nigeria Seyi Shay, amesema tayari amefunga ndoa.

Kujibu swali kutoka kwa shabiki wake, Seyi amesema harusi yake ilifanyika kitambo, licha ya yeye hakuwahi kuwa na mipango ya kuolewa, bali alitaka kupata watoto pekee.

"Harusi yangu tayari ilifanyika. Mimi ni mwanamke niliyeolewa, nimefungwa," amesema

## Halima ahofia waume za watu

MWIGIZAJI mkongwe wa Nollywood, Halima Abubakar, amewashauri wanawake wajiepushe na tabia za kujihusisha kimapenzi na waume za watu.

Aliongeza kuwa wanawake wanapaswa kutengeneza biashara ya kando na kuacha waume za watu na kuwashauri waepuke wanaume walioolewa na kukataa kuwa vifaranga wa pembeni.

Mwaka jana, mwigizaji huyo alidaiwa kutoka kimapenzi na Mtume Johnson Suleman wakati hali yake ya kiafya ilipokuwa mbaya.





## Mradi kunufaisha wakulima 8,000

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

WANAWAKE na watoto 26,943 mkoani Arusha, wanadaiwa kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa mwaka 2022, jambo ambalo limefanya kuwapo kwa ongezeko kubwa la vitendo hivyo.

Akizungumza jana kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, katika maadhimisho ya wanawake, Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, alisema idadi hiyo ni kubwa kutokana na namna ambavyo vitendo hivyo vimekuwa vikipingwa.

"Bado kuna tatizo la ukatili wa kijinsia ukilinganisha na namna tunavyopinga na kuukataa ukatili huo na vitendo hivi vinahitaji kupigwa vita kwa hali ya juu na ikiwezekana kusiwapo kabisa hata kama idadi itakuwa ndogo,"alisema.

Akisoma hotuba hiyo iliyoandaliwa na mkuu wa mkoa alisema kati ya watu hao 26,943 waliofanyiwa ukatili wa kimwili na kuripotiwa ni 8,647, huku walifanyiwa unyanyasaji wa kisaikolojia ni 12515 na 5781 wamefanyiwa ukatili wa kingono.

Hata hivyo, aliwataka wanawake kuvalia njuga suala la maadili alisema kuiga utamaduni wa nje umewaathiri wazazi katika malezi na watoto kwa ujumla jambo ambalo alilikemea kwa nguvu zote huku akiwataka kuwa na kiasi katika mambo ya kuiga.

Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Joshua Nassari, alisema wanawake hawana jambo dogo, hivyo wakiamua kuvalia njuga suala la ukatili, linaweza kwisha kabisa na aliwataka kuungana kupinga vitendo hivyo.

"Wanawake hawanaga shughuli ndogo ndugu zangu wakiamua jambo lao watahakikisha mpaka limekamilika hapo ndiko wataridhika kwa kuwa limefanikiwa " alisema Nassari.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Mkoa wa Arusha, Flora Zelothe, alisema wanaume wameacha majukumu yao na kuwaachia wanawake mzigo wa malezi.

"Ndugu zangu tushirikiane katika suala la malezi ili kuleta usawa wa kijinsia ,wanaume acheni kukimbia majukumu yenu na kuwaachia wanawake pekee," alisema Zelothe.

# Mfumo ushirikishwaji madini wazinduliwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, amezindua mfumo wa ushirikishwaji wa Watanzania katika sekta ya madini na wa utoaji wa huduma kwenye jamii unaofanywa na migodi ya madini.

Dk. Kiruswa alifanya uzinduzi huo jana kwenye jukwaa la pili la utekelezaji wa ushirikishwaji wa Watanzania katika sekta ya madini linaloendelea jijini Arusha, lililokutanisha kampuni za uchimbaji wa madini, watoa huduma kwenye migodi na taasisi za kifedha.

Alisema mfumo huo utawezesha kampuni za uchimbaji wa madini na watoa huduma kwenye migodi ya madini kuwasilisha nyaraka mbalimbali kwenye uwasilishaji wa mipango ya ushirikishwaji wa Watanzania katika sekta hiyo, utoaji wa huduma kwa jamii kwenye migodi kwa njia ya kielektroniki badala ya kutumia nakala ngumu kama ilivyokuwa awali.

Pia alisema mfumo pia utarahisisha shughuli ya uchakataji wa maombi yanayowasilishwa tume ya madini na majibu ya maombi kutolewa kwa wakati na wataalam kutoka kwenye tume hiyo.

Kuhusu mafanikio ya maboresho ya sheria ya madini yaliyochangia kutungwa kwa kanuni za ushirikishwaji wa Watanzania katika sekta ya madini, alisema pamoja na mabadiliko kufanyika imesaidia kuchochea ongezeko la fursa mbalimbali ikiwamo kutoa ajira na nafasi za mafunzo.

"Ajira kwa Watanzania katika migodi mikubwa zimeongezeka kutoka 6,668 mwaka 2018 hadi 15,341 mwaka 2022 na wananchi wamepata mafunzo mbalimbali ya kujengewa uwezo wa kufanya kazi kwa kuwa baadhi ya shughuli zilikuwa zinafanywa na wageni. Mwaka 2022, wananchi 8,066 walipatiwa mafunzo katika sekta ya madini na kujengewa uwezo katika utendaji kazi na Sh. bilioni 3.4 zilitumika," alisema.

Naibu Waziri alitaja mafanikio mengine yaliyopatikana kuwa ni ongezeko la ununuzi wa ndani ya nchi na kwamba mwaka 2022 Dola za Kimarekani bilioni 2.22 sawa na asilimia 97.4 ya ununuzi wa kampuni za madini ulifanyika kwa kutumia kampuni za Watanzania kulinganisha na Dola za Kimarekani milioni 238.71 sawa na asilimia 46 kwa mwaka 2018.

Pia alisema kumekuwapo na ongezeko la watoa huduma kwenye migodi ya madini kwa mwaka 2022 hadi kufikia 1,386 sawa na asilimia 81 kulinganisha na mwaka 2018 ambapo kulikuwa na watoa huduma 623.

Kamishna wa Tume ya Madini, Janet Lekashingo, alisema serikali kupitia tume hiyo, bado inaendelea kutoa elimu katika mikoa kuhusu ushirikishwaji wa Watanzania katika sekta hiyo ili wananchi wengi washiriki kwenye shughuli za utoaji wa huduma kwenye migodi ya madini.



Meneja wa Kiwanda cha chai Mponde, Sane Kwilabya (kulia), akitoa maelezo kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, kuhusu kazi ya uchakataji wa chai, walipotembelea kiwandani hapo, wilayani Lushoto, mkoani Tanga juzi, ili kuona uwekezaji uliofanywa na Serikali kupitia taasisi zake za PSSSF kwa ushirikiano na wabia wengine. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, CPA Hosea Kashimba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 2.2/ - za UVIKO- 19 zapaisha utalii

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, amesema Sh. bilioni 2.2 za mapambano dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya maboresho ya makumbusho ya malikale zimefanya kazi nzuri, hivyo kusaidia kuutangaza utalii kwa kiwango cha juu.

Masanya aliyasema hayo jana jijini hapa wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilipotembelea miradi ya UVIKO- 19 katika makumbusho ya Azimio la Arusha na elimu viumbe Arusha.

Alisema bado kunahitajika maboresho zaidi ili kuweka historia vizuri ya uhifadhi kwa njia ya malikale kupitia majumba ya makumbusho yaliyoko nchini.

Hata hivyo, alisema makumbusho yanaendeshwa kwa kusuasua kutokana na ufinyu wa bajeti ambapo kwa sasa wamejipanga kuweka kipaumbele kufanya maboresho mbalimbali kuhakikisha makumbusho hayo yanavutia na kuleta watalii wengi zaidi.

"Serikali imeweka mikakati mbalimbali kuhakikisha maeneo yote yaliyosahaulika yanaboreshwa yawe na mwonekano wa kisasa kwa kuwa itakuwa moja ya njia ya kuongeza mapato na idadi ya watalii wanaotembelea maeneo hayo," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Makumbusho ya Taifa, Dk. Oswald Masebo, alisema alitoa shukrani kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwekeza katika sekta hiyo.

Pia alisema wamepokea maelekezo na mapendekezo na watakwenda kufanyia kazi kwa kujipanga wenyewe na kufanya mazoezi makubwa.

Aidha, aliiomba kamati hiyo kuongeza bajeti ya kutosha kwa ajili ya shirika kwa lengo la kuboresha zaidi miundombinu mbalimbali na kufanya marekebisho makubwa.

Mkurugenzi wa Makumbusho ya Azimio la Arusha, Dk. Gwakisa Kamatula, alisema Sh. milioni 112 zilitengwa kwa ajili ya maboresho na ukarabati wa Azimio la Arusha na mradi umekamilika kwa asilimia 100.

Mkurugenzi wa Makumbusho ya Elimu Viumbe, Arusha, Christina Ngereza, alisema Sh. milioni 272 zilitolewa na serikali kupitia fedha za UVIKO-19 kwa ajili ya miradi minne ya makumbusho ya elimu viumbe Arusha .

Alisema miradi hiyo ni onyesho la tembo na wanyama watano wakubwa ,onyesho la wanyama aina ya reptilia, uboreshaji wa maabara ya baiolojia2 na uboreshaji wa stoo ya baiolojia.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Timothy Mnzava, alisema kamati iko tayari kutoa fedha endapo Wizara na Makumbusho watatoa maombi kwa kuwa wameonyesha uzalendo katika kufanyia kazi fedha walizopewa.

MAKALA

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Vituko vya timu za mitaani zamani

## -Kiwango kikubwa kuliko Ligi Kuu ya sasa, usela mwingi, ngumi nje nje

Na Adam Fungamwango

KWA sasa timu za mitaani hazina nguvu sana kama zile za miaka ya 1980, hadi mwishoni mwa miaka ya 1990.

Ni miaka ambayo soka la Tanzania lilikuwa juu sana, ambalo lilipamba moto miaka ya 1960, kiasi cha nchi hii kuwa juu sana kimichezo.

Leo tutaziangalia klabu na timu zao za mitaani, ambazo mashabiki wake mara nyingi huwa ni majirani na wakazi wa maeneo yanayozunguka hizo timu. Hufanya kila njia kuzisaidia ili kufanya vizuri. Na zilikuwa na mashabiki wengi waliokuwa wakiambatana na timu hizo kwenda uwanjani. Wapo waliokuwa mashabiki wa kawaida na wengine hawakuwa wa kawaida.

Moja ya timu maarufu sana Dar es Salaam miaka ya 1980, hadi katikati ya miaka ya 1990, ni 'Kiboko Msheli' Klabu hii ya mpira makao makuu yake yalikuwa Magomeni Makuti.

Ilikuwa maarufu siyo kwa ajili ya mpira tu uwanjani. Ila ilikuwa na mashabiki wakorofi na wababe.

Walikuwa na uwezo wa kufanya kitu chochote na wakati wowote ule, sehemu yoyote ile.

Kwa wakazi waliokuwa wanaishi maeneo ya kuzunguka Magomeni, kama Tandale, Manzese, Mwananyamala, Sinza, Kigogo, Mburahati, hata kama siyo mashabiki wa soka walilazimika kujua ratiba ya mechi za mchangani ambazo Kiboko Msheli watacheza.

Siyo kwa sababu walikuwa ni mashabiki wa timu hiyo, ila kujihami kiusalama na mali zao.

Ikifika saa nane mchana, basi wafanyabiashara watafunga maduka, na sehemu zote za biashara zitafungwa, kuwapisha mashabiki wa timu hiyo ambao walikuwa wakitoka kwa maandamano kutoka klabuni, kwenda kucheza mechi zao, za vikombe mitaani, na kurudi.

Ubabe wa mashabiki hao haukuwa mitaani tu, bali hata uwanjani. Si mara zote mechi zao zinamalizika kwa dakika 90. Mashabiki wao wako tayari kufanya chochote wanapoona mwamuzi anawaonea.

Timu zingine zilizovuma ni Boom FC na Ashanti zote za Ilala. Ashanti ni timu maarufu kuliko Boom kwa sasa kwa sababu imeshacheza Ligi Kuu.

Timu hizi ni hasimu na upinzani wao ni kama Simba na Yanga miaka hiyo, mechi ikichezwa Uwanja wa Karume kunakuwa na ulinzi mkali sawa na 'dabi' ya Kariakoo.



Ukiachana na Kiboko Msheli, Boom na Ashanti timu zilizoongoza kuwa na mashabiki wababe, timu nyingi za mitaani zamani zilikuwa na wababe wao ambao walikuwa wakiwalinda wachezaji na mashabiki wao wanapoenda kucheza mechi dhidi ya fujo zozote zitakazotokea dhidi yao, iwe nyumbani au popote watakapokwenda kucheza.

Ndiyo maana utaona kila timu wakati huo ilikuwa wa watemi wao maarufu, japo hata mmoja. Naweza nikasema kuwa soka lililokuwa likipigwa mitaani au viwanja mbalimbali nchini, ni la kiwango cha juu kuliko hata baadhi ya mechi za Ligi Kuu kwa sasa.

Hizi ni baadhi ya timu zilizovuma sana miaka hiyo ya 1980, hadi katikati ya 1990 Dar es Salaam na mikoani mbalimbali nchini.

Tunaanza na, Abajalo na Sinza Stars zote za Sinza, Milambo ya Mabibo, Sifa Politan ya Mtoni, Six Battalian, Black Septemba ya Tandika, Faru Dume na Las Vegas za Manzese, Gerezani Star ya Kariakoo, na Bongoyo FC ya Msasani.

Zingine ni Sea Breeze, Future ya Manzese, National ya Tandale, Chafosi Chaigoda ya Bagamoyo, Wacheche ya Ilala, Nevada ya Tandale, Kagera Rangers ya Manzese, Magomeni Kondoa FC, Les Leopard, Nzige Army, Sakramento ya Temeke, halafu kuna Batafongo ya Temeke Kota.

Halafu kulikuwa na timu za Shavee, Briston City, Vive Style, Polisalio, Black Six, Palestine, Uruguay, Great Olympic, Super Mzamba, Seven Blue Star, Opec, Berlin ya Tandika, Kitintale ya Bombom Kijiwe Samli, Santiago Chile ya Buguruni, African Temeke na Good Hope zote za Temeke, Avengers ya Mwenge, Keko Staff.

Kulikuwa na timu za Black People ya Majumba Sita Ukonga, TP Ibo au maarufu kwa jina la 'Kumkomanyani Giladi', TP Vita ya Kipawa, Msikate Tamaa na Mogo FC.

Kawe kulikuwa na timu za Ukwamani FC na Kawe Rangers, Mwananyamala kulikuwa na timu za Flamingo FC na Bonde FC, pia kulikuwa na timu za Santos, Pool England, Shangwe ya Ilala, Evarton, Ajax, Maputo, Osibisa, Bungoni Fresh, Shekilango DC, New Kenda ambayo ni timu ya Jeshi la Wananchi, Sifa United iliyowatoa Madaraka Selemani na mdogo wake Idd Selemani hadi kuja kuichezea klabu ya Simba.

Care Boys ilikuwa ni timu ya eneo ya Kinondoni Biafra, lakini kulikuwa na timu za Eleven Killers na Ugimbi United zote za Kurasini, Ngurumo na Ukombozi zote za Kigogo Luhanga, Machava FC, Nondo, TP Nyundo, Shoka Afrika zote za Mwananyamala, Batafongo ya Tandaka na Asanta Tololo ya Kariakoo na Al Aswan pia ya Kariakoo.

Mikoani nako hakukuwa nyuma, kulikuwa na Jamaica ya Morogoro, Mau Mau ya Chumbageni Tanga, Sungura FC ya Kyela Mbeya, Ombwezi ya Singida, Waya Mkali, Home Boys, Esso Arusha na Ololo Rangers zote za Arusha.

Pia kulikuwa na timu za Kiloleni Rangers, Ibadan na Torabora, zote za Tanga.

Hizi ni chache tu zilizokuwa zikisababisha mashabiki kujaa viwanjani kwenda kuzishangilia timu zao. Mbali na baadhi ya matatizo na changamoto za hapa na pale, lakini kulikuwa na burudani kubwa kuangalia timu hizo, vituko na mbwembwe za mashabiki wao.

Hapa umeikumbuka timu gani? na tuorodheshee timu maarufu ya mtaani kwako iliyotamba enzi hizo ambayo haikuorodheshwa na watemi wao.

**Tuma meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

## Raia wazidi kuandamana Israel

**TEL AVIV,** ISRAEL

MAANDAMANO makubwa yanaendelea kufanyika nchini Israel, wakati Waziri Mkuu, Benjamin Netanyahu anafanya ziara nchini Ujerumani.

Watu wameingia barabarani kuandamana kupinga mageuzi yenye utata ya mahakama.

Maandamano hayo yanafanyika kwenye sehemu mbalimbali za mji wa pwani wa Tel Aviv.

Waandamanaji walipambana na polisi, baadhi yao walizuia njia inayoelekea kwenye mji wa Jerusalem.

Watu wengine wamepanga kufanya maandamano, wakati wengine wamejikusanya mbele ya ubalozi wa Ujerumani mjini Tel Aviv.

Rais wa Israel, Isaac Herzog, alipendekeza kuwepo mwafaka ili kuleta suluhisho la mgogoro huo.

Hata hivyo, Netanyahu alilipinga pendekezo hilo kabla ya kuanza ziara ya kwenda nchini

## Raia wampa shinikizo rais Macron

**PARIS,** UFARANSA

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, anakabiliwa na shinikizo la maandamano yanayomtaka kufuta uamuzi unaotajwa kuwa usio wa kidemokrasia baada ya kuidhinisha mageuzi tata ya pensheni bila ya kura ya bunge.

Hatua ya kutumia mamlaka maalum ya kikatiba kupitisha sheria bila kura ya bunge, iliashiria kuwa serikali haina wingi wa kura.

Sheria hiyo imeongeza umri wa kustaafu kutoka miaka 62 hadi 64, mabadiliko ambayo yamekumbwa na upinzani mkali nchini kote.

Baraza la Seneti liliidhinisha mswada huo mapema jana, lakini kusitasita kwa wabunge wa upinzani wenye siasa za mrengo wa kulia kumuunga mkono Macron, kulionyesha kushindwa kwa serikali kuupitisha mswada huo bungeni.

Huduma ya usafiri wa treni, masomo shuleni, huduma za umma na bandarini zilisimama tangu Januari baada ya kuathiriwa na migomo ya kupinga mageuzi hayo.

**DW**

# Kamanda aliyetoa siri Ukraine, apata adhabu kushushwa cheo

**KYIV,** UKRAINE

KAMANDA wa kikosi cha jeshi la Ukraine Anatoly, maarufu kwa jina la "Kupol", ameshushwa cheo baada ya kutoa siri ya kushindwa vita katika mji wa Bakhmut.

Gazeti la Marekani la Washington Post, lilipata taarifa hizo kutoka kwa Kupol, ambaye alisema vikosi vya Ukraine vimeshindwa vibaya katika vita hiyo.

Taarifa za kushushwa cheo kwa mwanajeshi huyo zimetolewa na gazeti la Ukraine, linaloitwa Ukrainian Pravda.

Taarifa ya mwanajeshi huyo ilichapishwa baada ya kufanya mazungumzo na kundi la waandishi wa habari wa Marekani, ambao walichapisha taarifa hiyo tarehe 13 Machi, kuhusu hali halisi katika eneo la Bakhmut, ambako mapigano yanaendelea dhidi ya vikosi vya Russia.

Alidai kuwa kushindwa kwa jeshi la Ukraine katika mapigano ya Bakhmut kulitokana na kupungua kwa idadi ya wanajeshi, jambo ambalo awali liliangaliwa kama faida ya Ukraine ikilinganishwa na Russia.

Matokeo yake , baadhi ya maofisa wa jeshi walianza kuhoji utayari wa nchi hiyo kukabiliana na vita hiyo siku zijazo.

Miongoni mwa mambo mengine , kamanda huyo alisema kuwa takriban wanajeshi 100 kati ya 500 katika kikosi chake waliuawa na wengine 400 walijeruhiwa katika mashambulio ya Bakhmut.

Mwakilishi rasmi wa kikosi cha anga cha Ukraine, Valentin Shevchenko, katika mahojiano na gazeti la Ukraine la Ukrayinska Pravda, alisema taarifa zilizotolewa na mwanajeshi huyo zilizidi makadirio na sio za kuaminika na alisema watafanya uchunguzi zaidi kuhusu taarifa alizozitoa.

Wakati huo huo, Poland imesema itatuma ndege nne za kivita za aina ya Mig jetza, zilizotongenezwa enzi ya Usovieti. Endapo itatuma ndege hizo, itakuwa nchi ya kwanza kutoka mwanachama wa Nato kupeleka ndege zake nchini Ukraine, tangu Russia ianze uvamizi wake.

Rais wa Poland Andrzej Duda, alisema kwamba ndege hizo zitapelekwa katika siku zijazo, na nyingine zitapelekwa baadaye.

Ingawa msada huo utapokelewa vizuri, ndege hizo hazitarajii kuleta mabadiliko yoyote katika vita.

Naibu spika wa bunge la Ukraine Olena Kondratyuk, alisema kuwa anatumaini nchi zingine zitafuata mfano wa Poland.

Nchi nyingine za Nato zinaangalia uwezekano wa kutuma ndege zilizotengenezwa enzi hizo ambazo marubani wa Ukraine wamefunzwa kuzitumia . Awali Ukraine, iliyaomba mataifa ya Magharibi kuipatia ndege za kisasa za aina ya jeti kama vile F-16.

Uingereza inawapatia mafunzo marubani wa Ukraine kuhusu uendeshwaji wa ndege zenye viwango vya NATO.

**BBC**




Raia wakiandamana katika mitaa ya jiji la Paris kupinga sheria ya kuongeza umri wa kustaafu nchini Ufaransa jana. **PICHA: AFP.**

# Ruto ateua manaibu waziri 50

**NAIROBI,** KENYA

RAIS wa Kenya William Ruto, amewateua manaibu waziri 50 ambao wamepewa kusimamia wizara 22.

Kwenye orodha hiyo iliyotangazwa kupitia taarifa ya Mkuu wa Utumishi wa Umma, Felix Koskei, idadi kubwa ya manaibu mawaziri hao ni wanasiasa wa Muungano wa Chama tawala Kenya Kwanza walioshinda kwenye uchaguzi mkuu uliopita. Miongoni mwao ni aliyekuwa Gavana wa Kaunti ya Nairobi Evans Kidero, Seneta mteule wa zamani Millicent Omanga, aliyekuwa mbunge wa Starehe Margaret Wanjiru na mbunge wa zamani wa Rarieda Mhandisi Nicholas Gumbo.

Uteuzi huo ulioidhinishwa na Tume ya Utumishi wa Umma, umepokelewa kwa hisia tofauti na Wakenya.

Watu wengi katika mitandao ya kijamii wamehoji utashi wa Rais Ruto wa kutimiza ahadi yake aliyoitoa kwenye kampeni ya kuwateua wananchi wa tabaka la chini ambao aliwaita 'Mama Mboga na Boda Boda'.

Serikali inakosolewa pia kwa kushindwa kupunguza mzigo wa kuajiri maofisa wengi serikalini wanaolipwa fedha nyingi za walipa kodi.

Baadhi ya wizara zimetengewa manaibu waziri zaidi ya wawili. Serikali iliyopita ya Rais Uhuru Kenyatta, ambayo Rais wa sasa William Ruto alikosoa vikali kwa teuzi nyingi alizozitaja mzigo, kulikuwa na mawaziri 23.

Katika ukurasa wake wa Twitter,Naibu wa Rais Rigathi Gachagua, ametetea uteuzi huo akisema wizara zina masuala mengi ambayo yanahitaji kushughulikiwa.

Walioteuliwa kuchukua wadhifa huo wa manaibu waziri haujaanishwa kama inavyotaka Katiba ya Kenya, lakini, watapigwa msasa na bunge kabla ya kuanza rasmi kutekeleza majukumu yao.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SULTAN MBWANA KUSAGE** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **TVS** yenye usajili namba: **MC 122 DMG,** CHASSIS NAMBA: **MD625AF4XN1D05948** na ENGINE NAMBA: **DF4DN1X05550.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi POLISI TAARIFA: **DAR/CEN/RB/87707/20232.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJI NA PIKIPIKI

**SAIDY SHWAHIBU MBWAMBO** anatangaza kupotea kwa kadi za bajaji aina ya **WANHOO** zenye usajili namba **MC 393 BVZ, MC 995** na aina ya TVS yenye usajili namba **MC 788CYD** na kadi ya pikipiki aina ya **BOXER** yenye usajili namba **MC 818 AZK.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/KIM/RB/99295/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SHAMIM A KADEGHE** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ZA PIKIPIKI **(BOXER)** Zenye namba za usajili **MC 387 BJG, MC 416 BJG na MC 323 BQG.** Chasis Namba: **MD2A21BZ8GWC97913 na MD2A21B24GWC97889** Engine Namba: **PFZWGC21957, PFZWGC21879** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/96711/2023.**

**3 FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMNISTRATION CAUSE NO, 252 OF 2023**
**In the Matter of the Estate of the Late OMUNDA ANTONY GAMA**

**And**

**In the matter of Application for letter of administration by**
**FELIX EDWARD GAMA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above –named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **3th day of May 2023.**
Dated at DAR ES SALAAM this **16th day of March 2023**

Senior Resident Magistrate

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA RUFAA NA. 332 YA MWAKA 2022**
**NYANYA MOHAMED...........MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MUDRI A. MBELEKO**
**ABDALLAH JUMA SEIF .............WAJIBU MAOMBI**

**KWA:**
**MUDRIA A. MBELEKO**
**ABDALLAH JUMA SEIF**
**DAR ES SALAAM**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mwombaji aliyetajwa hapo juu amefungua shauri dhidi yako, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati ya madai zinazopatikana katika mahakama hii, unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii, wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako ambaye anaruhusiwa kisheria siku ya tarehe 4/4/2023 saa tatu (3:00) asubuhi mbele ya Mhe. Jaji E.Y. Mkwizu kujibu madai hayo dhidi yako. Unaagizwa kuleta vielelzo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia katika utetezi wako siku hiyo.
**ANGALIA:**
Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na mahakama ikathibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.
HATI hii imetolewa kwa MKONO wangu na CHAPA ya mahakama leo hii tarehe 10th mwezi March, 2023.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
KANDA YA DAR ES SALAAM

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**
**SHAURI LA RUFAA JINAI NA. 61/2022**
**Asilia Shauri la jinai 158/2021, Mahakama ya Wilaya Chunya**

**JAMHURI.................................MRUFAA**
**DHIDI YA**
**OBEDI MWANI JEMBE LAZARO.....MJIBU RUFAA**

**KWA BWANA: JUMA TANGANYIKA**
**POPOTE ULIPO...........TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

Unaamuliwa na mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakamani tarehe **20/03/2023** siku ya Jumatatu saa 3:00 asubuhi bila kukosa
**ELEWA KWAMBA,** ukikosa siku hiyo, shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa
Hati hii imetolewa na Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe **20/02/2022**

NAIBU MSAJI MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANTONY LUKALA NICHOLAUS** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.834 DSK.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KWA RB NAMBA **DAR/PHQ/RB/98767/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ANTHONY MASHENENE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC.365 DBF.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KWA RB NAMBA **KIS/RB/27/2023**

***OFISI ZA MATANGAZO***

***Mikocheni Industial Area,***

***Po.Box 31042, Dar es Salaam.***

***Mobile: +255 - 745 700 710.***

***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***

***Website: www.ippmedia.com***

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

# MTAKE MSITAKE-23

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kiburi cha kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja wa wasichana warembo kijiji hapo ni mmoja ya waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

"Ni kweli, kuanzia leo nawatangazia rasmi kuwa mimi ni mchumba wa Mary. Nilianza kumpenda tangu siku ya kwanza nilipomuona kwenye mkutano wa kijiji. Na hata siku niliyokutana naye mara ya pili na kumuokoa kwenye ajali ya pikipiki. Ingawa ni msiri, alianza kwa kunikataa, akaniambia kweli unanipenda, lakini nina mchumba anaitwa Enock. Kitu ambacho kilimfanya kuniambia siri yake kuwa Enock hakuwa mchumba halisi ni pale alipoona pamoja na kukataliwa, bado niliendelea kumpenda, kuwasiliana naye na sikuonyesha kukasirishwa kwa namna yoyote ile, au kumuacha na kuanza kufuata wanawake wengine ambao hawana wapenzi. Akanikutanisha na Enock. Kumbe ulikuwa ni mpango wao tu wa kuniweka karibu. Niliposikia kuwa hakuwa mpenzi wake kwanza sikuamini, halafu Enock mwenyewe akasema yeye anajivua, kwani Mary sasa amepata mpenzi halisi na yeye akarejea kwa mpenzi wake Amina. Nikamwambia kwanza endelea kwa sababu kuna mpango nataka kuufanya. Ikawa ni timu ya watu watatu. Nikawaambia na mimi kazi yangu niliyojia kwenye kijiji hicho, hapo ndipo tulipotengeneza mkakati huu uliofanikiwa kwa asiliamia 100."

Wengine sasa hawakutaka kusikia chochote walikuwa na shangwe tu ya kuwa huru, ardhi yao imerudi, kumbe Adel si kipofu, kumbe Adel ni mpelelezi aliyekuja kukirudisha kijiji mikononi kwa wananchi, halafu pia Enock si mchumba wa Mary na sasa kumbe Adel ndiye anakuwa mchumba halisi wa Mary.

"Naomba Mary usimame uje kwenye jukwaa hapa, uongee mawili matatu, halafu nikupe zawadi yako, ambayo itawatambulisha watu wote hapa kuwa mimi na wewe ni wachumba na nahitaji uwe mke wangu."

Maneno hayo yalifuatiwa na kelele za shangwe na vigelegele kutoka kwa kinamama.

Wakati Adel anakwenda jukwaani akiwa na miwani yake akiigiza upofu, Mary alionekana kama mtuhumiwa, lakini sasa amekuwa mtu mwingine kabisa. Mpenzi wa Adel, kama minong'ono iliyokuwa awali wakati ikiaminika ni mpenzi wa Enock.




**Mkutano ukabaki wa walinzi wawili tu, wote walikuwa wameshaondoka baada ya kuona usalama upo wa kutosha.**

Alipofika, akakumbatiana na Adel kwa nusu dakika, huku watu wote ambao walikuwa wakipiga shangwe, wakaanza pia kupiga makofi, na miluzi juu. Tayari wameshakuwa ni wakombozi wao.

Akapewa maiki na MC ambaye alikuwa ameichukua kutoka kwa Adel. Akaichukua akiwa kwenye tabasamu moja pana.

"Ndugu wanakijiji wenzangu, baba mama, kaka na wadogo zangu. Mimi mnanijua si mzungumzaji sana. Ila naomba tu niwaambie kitu."

"Sema mama." Zilisikika sauti zikimhimiza. "Kusema kweli wakati huu mpango tunaupanga na Adel niliogopa sana. Nilijiona kama ni mpango mikubwa sana na huenda isifanikiwe, na nilijichukulia kama mtoto wa kike ingekuwa ngumu kwangu. Adel alinibembeleza sana.

Lakini aliponiambia kwamba yeye ni Ofisa Usalama wa Taifa na yote anayoyafanya ni kwa sababu amekuja kukikomboa kijiji, nikaona sasa hapa kuna usalama.

Na hiki anachofanya na mimi nikimuunga mkono na mimi nitakuwa mmoja kati ya watakaotoa msaada. Haiwezekani mtu atoke mbali atake kutusaidia, halafu mimi nikatae. Lakini vile vile tayari mimi mwenyewe nilishaanza kumpenda..." Hakuendelea, kwani zilizuka kelele zingine kubwa zaidi za kushangilia, halafu baadaye zikapoa. "Ila tu hapa mwishoni nilipata matatizo sana, maana kila mtu aliniona mbaya kwa kumwagia mtoto wa watu tindikali, lakini nilivumilia tu. Aliponisaidia kwenye ajali ya bodaboda ambayo ilitaka kunipata, wiki moja baadaye aliniambia kuwa ananipenda na angetaka kuwa na mimi.

Nilimkatalia na kumwambia nina mchumba wangu Enock. Alikuwa hajui kama uchumba wangu mimi na Enock ulikuwa feki kwa ajili ya kumkwepa Usonzo asinifuatefuate. Alisononeka na kuumia, lakini hakuacha kuwasiliana na mimi tukiendelea na urafiki wetu tu wa kawaida.

Hakuonekana kunikwepa au kutaka mawasiliano na mimi na kufuata wasichana wengine. Hili lilinivutia sana na kuamini kweli huyu kaka ananipenda.

Nilivyoona hivyo nikaongea na Enock kumfahamisha kuwa sasa nadhani nimepata mpenzi halisi ambaye hivi karibuni nitamuweka hadharani.

Nikawakutanisha, wakawa marafiki, watu wakawa wanashangaa, eti mtu na mume mwenzake ni marafiki. Kumbe sisi tulikuwa na yetu. Rasmi nikamwambia Adel kinachoendelea. Mapenzi yangu mimi na yeye yakaanza na akaanza kunipa mipango yake ya kumhadaa Usonzo.

Kuanzia ya kujifanya nimemwagiwa tindikali, hadi kwenda kujipendekeza kwa Usonzo yeye akadhani kweli sasa nimemkubali, lakini kumbe ilikuwa ni kumuweka Adel karibu naye kwa ajili ya kumpeleleza na kweli akaingia mkenge. Mwisho wa yote nasema mimi mwenyewe nimekubali kuwa mchumba Mungu alijalia mume wa Adel." Vigelegele vikasikika kwa kinamama.

Wakati huo magari , likiwemo liliwawachukua watuhumiwa Usonzo na mwenyekiti Chale yalianza kuondoka na likabaki moja tu.

Mkutano ukabaki wa walinzi wawili tu, wote walikuwa wameshaondoka baada ya kuona usalama upo wa kutosha.

"Ndugu wanakijiji hapa sasa namalizia kwa kufanya tukio kubwa sana ambalo wote napenda mlishuhudie. Nataka kumpa zawadi kubwa sana mwanakijiji mwenzenu, binti yenu, dada yenu, mdogo wenu, mrembo Mary."

Aliingia kwenye mkono wa shati na kutoa kitu kinachong'aa hivi. Ni pete. Watu walipagawa kwa 'sapraizi' zinazoendelea kuonyeshwa pale.

Alikishika kidole cha Mary na kukivisha, tukio lililofuatiwa na shangwe ambazo zilichukua dakika tano kukoma.

"Mary, umefanya kazi kubwa sana. Wewe ni shujaa pia. Nakuvisha hii pete na nakuahidi mbele ya wanakijiji wenzao na wazazi wako kuwa nitakuoa." Akiwa amepagawa kwa furaha isiyo kifani kwa maneno ya .

"Sijui niseme nini bwana wangu, mfalme wangu, mkombozi wangu na shujaa na kijiji kizima. Umekuwa mwokozi wetu. Kwangu mimi wewe ni mfalme, nakuahidi nitakuwa ubavuni kwako milele, nakupenda sana."

Baada ya maneno ya Mary, shangwe ziliibuka upya, mambo yakawa yamekwisha. Sherehe ni kama zilianza upya. Sasa zikigeuka kama sherehe za 'send off' ya Mary ambaye sasa siku si nyingi ataolewa na Adel kabla ya kwenda kuishi Dar es Salaam.

**MWISHO**

# VILLA FC YAIVUA KIPANGA UBINGWA WA FA ZANZIBAR

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la Shirikisho Zanzibar (FA CUP), Kipanga FC wameondolewa katika hatua ya 32 bora ya michuano hiyo baada ya kupokea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Villa FC inayoshiriki Ligi ya Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mchezo huo ulioacha majonzi na maumivu kwa mashabiki wa Maafande wa Kipanga ulichezwa kwenye Uwanja wa Amaan, juzi.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Kipanga, Khamis Hassan, alisema matokeo hayo yamewasikitisha na kuwapa huzuni kwa sababu hai kuwa malengo yao.**

Hassan alisema baada ya kushindwa kufanya vizuri katika Ligi Kuu Zanzibar msimu huu, mipango yao mikubwa ilikuwa ni kutetea ubingwa wa michuano hiyo, lakini sasa ndoto hizo zimeyeyuka mapema.

Kocha huyo alisema hayakuwa matokeo mazuri kwa upande wao kutokana na maandalizi waliyofanya na kilichobakia ni kuhakikisha wanafanya vizuri katika michezo ya Ligi Kuu Zanzibar iliyobakia.

"Tuseme kama malengo yetu yamezimika ghafla, haikuwa matarajio yetu kabisa, lakini pengine haikuwa rizki yetu sisi kufanya vizuri katika msimu huu, hivyo tutajipanga kwa ajili ya msimu ujao,"Hassan alisema.

Kuhusu mchezo huo, Hassan, alisema wachezaji walicheza vizuri lakini siku zote timu za Ligi kuu zinapokutana na timu za madaraja ya chini,hali ya mchezo hubadilika. "Timu za madaraja ya chini hucheza kwa kukamia ili kupata matokeo mazuri dhidi ya timu za madaraja ya juu (Ligi Kuu), tutasema tumeumia, lakini tumekubali matokeo," aliongeza.

Timu nyingine iliyoaga mashindanao hayo ni Kiembe Samaki ambayo ilifungwa penalti 3-2 na Kundemba FC.



Mashabiki wa Yanga wakishiriki zoezi la kuchangia damu katika Hospitali ya Mloganzila kwa ajili ya kupata tiketi za bure ili kushuhudia mechi ya Kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya US Monastir kutoka Tunisia itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# *Yanga Princess yaizindua Mkwawa*

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Msaidizi wa Yanga Princess, Fred Mbuna, akisema timu yake ilishindwa kufuata maelekezo vyema na kuambulia sare, Kocha Mkuu wa Mkwawa Queens, Damian Mussa, ametamba kikosi chake kimeamka na anatarajia kupata matokeo mazuri kwenye mechi zinazofuata.

Yanga Princess iliambulia suluhu dhidi ya Mkwawa Queens inayoburuza mkia katika Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Mbuna alisema matokeo hayo yalitokana na wachezaji wake kushindwa kufuata maelekezo waliyowapa na kupoteza nafasi za kufunga mabao walizozipata.

"Tatizo ni wachezaji, wamecheza walivyoweza, tumepoteza nafasi nyingi ambazo tulizifanyia kazi mazoezini, hata hivyo hatujapoteza, tumepata suluhu, tutaenda kujipanga kwa ajili ya mechi nyingine. Hii ni ligi na mechi bado zipo nyingi, huwezi kusema tumepoteza matumaini ya kutwaa taji, bado tunaukimbiza ubingwa," alisema Mbuna.

Naye Mussa alisema kwa sasa wachezaji wake wameanza kuelewana na anaamini mchezo unaofuata watapata ushindi.

"Tumetoa sare na timu kubwa, nzuri inayocheza vizuri, sasa tumeanza ligi, kila timu itakayokuja mbele yetu, Fountain Gate Princess wanaosumbua tutakaocheza nao mechi ijayo wajiandae," alisema kocha huyo.

Simba Queens ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 26 sawa na Fountain Gate Princess, nafasi ya tatu inashikiliwa na JKT Queens yenye pointi 25 na Yanga Princess ipo kwenye nafasi ya nne ikiwa na pointi 21.

## Prisons yaitisha Ruvu Shooting

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Prisons imesema mechi dhidi ya Ruvu Shooting itakayochezwa Aprili 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine, Mbeya ndiyo itaanza kuamua hatima yao ya kubaki katika Ligi Kuu au kushuka daraja, imeelezwa.

Ofisa Habari wa Prisons, Jackson Mwafulango, alisema jana wameandaa mikakati kabambe ya kuhakikisha wanashinda mechi hiyo.

Mwafulango alisema wanajua Ruvu Shooting haipo katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi, lakini watawasamehe kwa sababu nao wapo kwenye mkakati wa kuhakikisha timu yao inabaki Ligi Kuu.

"Prisons ni moja ya timu nzuri, lakini upepo mbaya ulipita kati na sasa timu inaonekana imekaa vyema, tunamheshimu Kocha Mbwana Makata na benchi lake la ufundi, tunaiheshimu Ruvu Shooting kama timu nzuri iliyokamilika ndani ya nje ya uwanja, lakini watatusamehe kwa sababu tunajua tukishinda mechi hiyo, itaturahisishia kazi kuelekea mechi zinazofuata," alisema kiongozi huyo.

Hata hivyo alimsifu Kocha, Abdallah Mohamed 'Bares' kwa kuibadilisha timu hiyo ambayo sasa imerejesha matumaini ya kusalia katika Ligi Kuu Bara.

## Wachezaji waitwa Lugalo Open 2023

**Na Shufaa Lyimo**

WANAMICHEZO zaidi ya 100 kutoka sehemu mbalimbali wamejiandikisha kushiriki mashindano ya wazi ya gofu (NBC Lugalo Open ), yatakayofanyika Machi 25 na 26, mwaka huu hapa Dar es Salaam.

Nahodha wa klabu ya gofu ya Lugalo, (TPDF), Japhet Masai, aliliambia gazeti hili maandalizi kuelekea mashindano hayo yanaendelea vyema.

"Mpaka sasa tumepokea maombi kutoka kwa zaidi ya washiriki 100 ambao wamejiandikisha ili kushiriki, tunaomba kila mwanachama wa klabu yoyote aliyesajiliwa aje kujiandikisha, hakuna kiingilio," alisema Masai.

Nahodha huyo alisema mashindano ya mwaka huu yanasimamiwa na Chama cha Gofu Tanzania (TGU), na wanawataka wazazi na walezi kuwapeleka watoto wao kujiunga na klabu hiyo.

"Tunashauri wazazi walete watoto wao hapa ili wafundishwe jinsi ya kucheza mchezo huu, tangu tumeanza kufundisha watoto wadogo tumepata idadi kubwa ya vijana ambao miaka ijayo watatunda Timu ya Taifa," Masai aliongeza.

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMTAKA JUDE

KLABU ya Manchester United iko tayari kuwasilisha dau la kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19 kutoka Borussia Dortmund. (***Telegraph***)

### MADDISON NA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inataka kumpa kipaumbele kiungo wa Leicester City, James Maddison, katika msimu huu wa joto huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 akisemekana kutaka kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya. (***The I***)

### DELE MAMBO MAGUMU

MUDA wa mkopo wa Dele Alli katika klabu ya Besiktas hautafanywa kuwa wa kudumu msimu wa joto, huku Everton wakitarajiwa kusitisha mkataba wa kiungo huyo mwenye umri wa miaka 26. (***Football Insider***)

### HENRY AIKATAA UFARANSA

THIERRY Henry amekataa nafasi ya kuwa kocha mkuu wa timu ya wanawake ya Ufaransa. (***Le Figaro***)

### VEIGA AGEUKA LULU

MANCHESTER United, Newcastle United, Brighton na Brentford zimeonyesha nia ya kumnunua kiungo wa kati wa Hispania, Celta Vigo, Gabri Veiga, mwenye umri wa miaka 20 pamoja na klabu nyingine za Ligi Kuu England. (***90 Min***)

### MARCH KITAELEWEKA

WINGA wa Brighton, Solly March, mwenye umri wa miaka 28 anatazamiwa kusaini mkataba mpya na klabu hiyo wakati mkataba wake wa sasa ukitarajiwa kumalizika msimu huu wa joto. (***The Athletic***)

### NEVES MAMBO MAZURI

KLABU ya Wolves iko tayari kumpa mkataba mpya nahodha na kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ureno, Ruben Neves, mwenye umri wa miaka 26. (***90 Min***)

### COUFAL ANUKIA LEVERKUSEN

KLABU ya Bayer Leverkusen imeonyesha nia ya kumsajili beki wa West Ham na Timu ya Jamhuri ya Czech, Vladimir Coufal, mwenye umri wa miaka 30. (***Football Insider***)

### ROSE AJIFUA MAREKANI

MLINZI wa zamani wa Tottenham na Timu ya Taifa ya England, Danny Rose, mwenye umri wa miaka 32, anafanya mazoezi na klabu ya York City inayoshiriki Ligi Kuu Marekani. (***Sun***)

### VIEIRA ATIMULIWA PALACE

CRYSTAL Palace imetangaza kumfukuza kazi kocha wake, Patrick Vieira baada ya kushindwa kupata ushindi katika michezo 12. Palace haijapata ushindi wowote tangu mwaka 2023 ulivyoingia. Katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi ilichapwa bao 1-0 na Brighton.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA





# ODEGAARD AFUNGUKA KUFIKIRIA TAJI LA EPL

## Asema nguvu zote sasa zielekezwe katika mbio za kuwania kombe hilo ambalo...

**LONDON,** England

MARTIN Odegaard ameitaka Arsenal "kurejea kwa nguvu zaidi" baada ya kuondolewa katika mashindano ya Ligi ya Europa na Sporting CP hapo juzi, imeelezwa.

Penalti iliyokoswa na Gabriel Martinelli ilipelekea washikabunduki hao kutolewa katika mechi ya mkondo wa pili ya hatua ya 16 bora kwenye Uwanja wa Emirates, baada ya kutoka ya mabao 2-2 katika mchezo wa kwanza.

Matokeo hayo yanamaanisha Arsenal sasa wameshindwa kushinda mechi yoyote kati ya tano za mwisho za mtoano wakiwa nyumbani kwenye Ligi ya Europa tangu walipoifunga Valencia Mei, mwaka 2019.

Macho yote sasa yatakuwa katika kampeni ya Ligi Kuu England, ambapo Arsenal wanaogoza kwa pointi tano dhidi ya Manchester City zikiwa zimesalia mechi 11 kuchezwa, na Odegaard anataka timu yake kujibu mapigo dhidi ya Crystal Palace hapo kesho.

**"Nadhani tulifanya vya kutosha katika baadhi ya vipindi vya mchezo lakini mechi nyingi hatukuwa katika kiwango ambacho tunapaswa kuwa," alisema akiiambia BT Sport.**

"Sehemu ya mchezo tulifanya vizuri, katika mchezo mzima, hatukucheza soka letu bora zaidi. Ulikuwa mchezo mgumu mwishoni.

"Ni timu nzuri, tulijua hilo, tulijua sifa zao, na tulijiandaa, lakini nadhani ilikuwa zaidi juu yetu leo (juzi).

"Hatukucheza jinsi tunavyofanya kawaida, na labda hatukuweka nguvu kama kawaida. Hiyo inakatisha tamaa lakini sasa tunapaswa kuangalia mbele na kuwa tayari kwa Jumapili.

"Lazima tukumbuke umekuwa msimu mzuri sana, tumefanya mambo ya ajabu mwaka huu, bila shaka ni pigo kubwa kutoka kwenye mashindano haya, lilikuwa ni lengo kubwa kwetu, lakini tunatakiwa kutazama mbele.

"Lazima tuangalie Jumapili, turudi kwa nguvu zaidi na kuhakikisha tunamaliza vizuri kwenye ligi, hilo ndilo jambo pekee tunaloweza kufanya kwa sasa."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,090,5
MECHI KALI
SIMBA
VERSUS
HOROYA AC
1 | 1.73
X | 3.13
2 | 4.73
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TEN HAG AKUNWA NA KIWANGO CHA UNITED



**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag alisifu uimara wa kikosi cha Manchester United baada ya kushinda bao 1-0 ugenini dhidi ya Real Betis na akatania alifurahi hakuna mchezaji wake aliyetolewa nje kwa kadi nyekundu.

Bao la Marcus Rashford mapema katika kipindi cha pili lilithibitisha tofauti katika mchezo huo wa mkondo wa pili uliochezwa juzi wakati United ilipofuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Europa kwa jumla ya mabao 5-1.

"Nadhani wachezaji wote walifanya vizuri sana," alisema akiiambia BT Sport.

"Wale walioingia walifanya vizuri. Hatuna wachezaji 11 pekee, tuna kikosi."

Hata hivyo, licha ya kuzungumzia uimara wa kikosi chake, Ten Hag alifurahishwa na kutopoteza mchezaji yeyote katika hatua ya robo fainali.

Alipoulizwa kuhusu kipengele cha kilichompendeza zaidi cha ushindi huo, Mholanzi huyo alisema: "Hakuna kadi nyekundu, hakuna majeruhi. Tuna kikosi kikubwa."

"Nina furaha lakini tunapenda changamoto," Ten Hag alisema. "Tulijua hapo awali kwamba Betis ni timu nzuri sana. Tumeiona dhidi ya Real Madrid na dhidi ya Barcelona.

# *Alvarez aongeza mkataba hadi 2028*



**MANCHESTER,** England

JULIAN Alvarez amesaini mkataba mpya na Manchester City hapo juzi ambao utamweka hapo kwenye dimba la Etihad kwa msimu mmoja zaidi.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Argentina alijitolea kuongezewa mwaka mmoja, na kumaanisha amesajiliwa na City hadi mwisho wa msimu wa 2027-28.

Mchezaji wa zamani wa River Plate, Alvarez amefanikiwa kufunga mabao 10 katika mechi 33 alizoichezea City hadi sasa, akianza mara 14.

Anafanya kazi katika kivuli cha Erling Haaland, kwani Mnorway huyo anafurahia msimu wa kwanza uliovunja rekodi nchini England

Hata hivyo, City wana imani Alvarez mwenye umri wa miaka 23 tayari ana uwezo wa kung'ara zaidi katika kiwango cha juu zaidi.

Alvarez alisema baada ya kusaini mkataba huo: "Nimefurahishwa sana na msimu wangu wa kwanza hapa, lakini nina mengi zaidi ninaweza kufanya. Najua ninaweza kuwa bora zaidi, na City wananipa kila kinachohitaji ili kutimiza uwezo wangu. Sasa nina umakini mkubwa katika kuwa bora na kusaidia City kushinda mataji."

Txiki Begiristain, Mkurugenzi wa Soka wa City, alimuelezea Alvarez kama "mchezaji mchanga bora zaidi."

## HABARI MICHEZO

583,531/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.18/03/23 | 18:00 | Aberdeen FC vs Heart of Midlothian FC | 2.38 | 3.40 | 2.65 |
| 02.18/03/23 | 18:00 | Rotherham United vs Cardiff City | 2.55 | 3.15 | 2.65 |
| 03.18/03/23 | 18:00 | Stoke City vs Norwich City | 2.65 | 3.15 | 2.55 |
| 04.18/03/23 | 18:15 | Albacete Balompie vs Granada CF | 2.55 | 2.95 | 2.80 |
| 05.18/03/23 | 18:30 | Portimonense SC vs FC Vizela | 2.75 | 3.05 | 2.50 |
| 06.18/03/23 | 20:30 | Espanyol Barcelona vs RC Celta de Vigo | 2.75 | 3.05 | 2.50 |
| 07.18/03/23 | 20:45 | FC Emmen vs Sparta Rotterdam | 2.50 | 3.10 | 2.70 |
| 08.18/03/23 | 21:00 | Quevilly-Rouen Metropole vs FC Metz | 2.60 | 2.95 | 2.75 |
| 09.18/03/23 | 21:00 | Chamois Niort FC vs Stade Lavallois MFC | 2.60 | 3.00 | 2.70 |
| 10.19/03/23 | 14:15 | FC Groningen vs SC Heerenveen | 2.70 | 3.20 | 2.46 |
| 11.19/03/23 | 14:30 | Sampdoria Genoa vs Hellas Verona | 2.85 | 3.00 | 2.48 |
| 12.19/03/23 | 15:30 | Eintracht Braunschweig vs Hannover 96 | 2.46 | 3.30 | 2.65 |
| 13.19/03/23 | 16:30 | Excelsior Rotterdam vs SC Cambuur | 2.55 | 3.30 | 2.50 |
| 14.19/03/23 | 17:00 | ESTAC Troyes vs Stade Brest 29 | 2.70 | 3.20 | 2.45 |
| 15.19/03/23 | 18:15 | CA Osasuna vs Villarreal CF | 2.90 | 3.05 | 2.40 |
| 16.19/03/23 | 19:00 | FK Austria Wien vs SK Rapid Wien | 2.40 | 3.15 | 2.45 |
| 17.19/03/23 | 20:00 | Lazio Rome vs AS Roma | 2.60 | 2.95 | 2.75 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 18/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 5637 | Motherwell vs Rangers | 6.84 | 4.83 | 1.37 |
| 16:00 | 1377 | AS Vita Club vs Wydad Casablanca | 3.28 | 3.33 | 1.98 |
| 16:00 | 1596 | AL Hilal vs Mamelodi Sundowns | 2.55 | 2.85 | 2.55 |
| 16:00 | 3770 | Almeria vs Cadiz CF | 2.00 | 3.34 | 3.44 |
| 17:00 | 3374 | Monza vs Cremonese | 1.77 | 3.49 | 4.18 |
| 17:30 | 1180 | Hoffenheim vs Hertha BSC | 2.05 | 3.40 | 3.25 |
| 17:30 | 1205 | Augsburg vs Schalke 04 | 2.25 | 3.34 | 2.89 |
| 17:30 | 1825 | VfL Bochum vs RB Leipzig | 5.22 | 4.12 | 1.53 |
| 17:30 | 3154 | Stuttgart vs VfL Wolfsburg | 2.35 | 3.25 | 2.80 |
| 18:00 | 1219 | Watford vs Wigan | 1.72 | 3.39 | 4.69 |
| 18:00 | 1303 | Brentford vs Leicester | 1.92 | 3.49 | 3.54 |
| 18:00 | 1701 | Celtic vs Hibernian | 1.17 | 6.85 | 12.08 |
| 18:00 | 2431 | QPR vs Birmingham | 2.31 | 3.09 | 2.99 |
| 18:00 | 2474 | Reading vs Hull City | 2.75 | 3.15 | 2.45 |
| 18:00 | 2777 | Millwall vs Huddersfield | 1.50 | 3.76 | 6.42 |
| 18:00 | 2898 | Stoke City vs Norwich City | 2.34 | 3.20 | 2.85 |
| 18:00 | 3529 | Wolverhampton vs Leeds | 2.20 | 3.10 | 3.20 |
| 18:00 | 4116 | Aston Villa vs Bournemouth | 1.67 | 3.70 | 4.51 |
| 18:00 | 4186 | Livingston vs Ross County | 2.10 | 3.21 | 3.36 |
| 18:00 | 4263 | Aberdeen vs Hearts | 2.39 | 3.42 | 2.67 |
| 18:00 | 4302 | Rotherham vs Cardiff | 2.70 | 3.15 | 2.49 |
| 18:00 | 4783 | Middlesbrough vs Preston | 1.52 | 3.89 | 5.78 |
| 18:00 | 4918 | Blackpool vs Coventry | 3.09 | 3.19 | 2.21 |
| 18:00 | 5025 | Southampton vs Tottenham | 4.30 | 3.45 | 1.76 |
| 18:00 | 5801 | Dinamo Minsk vs Isloch | 1.60 | 3.73 | 4.87 |
| 18:00 | 5959 | Sunderland vs Luton Town | 2.59 | 3.14 | 2.59 |
| 18:15 | 1770 | Rayo Vallecano vs Girona | 2.01 | 3.30 | 3.45 |
| 18:15 | 5567 | Bodo Glimt vs Viking | 1.38 | 4.69 | 6.25 |
| 18:30 | 1524 | Utrecht vs GO Ahead Eagles | 1.71 | 3.75 | 4.20 |
| 18:30 | 5386 | Portimonense vs FC Vizela | 2.76 | 3.11 | 2.49 |
| 18:45 | 3944 | Orlando Pirates vs SuperSport Utd | 2.16 | 3.04 | 3.36 |
| 19:00 | 4133 | Toulouse vs Lille | 3.11 | 3.51 | 2.07 |
| 19:00 | 5549 | Simba vs Horoya AC | 1.73 | 3.13 | 4.73 |
| 19:00 | 5867 | Vipers SC vs Raja Casablanca | 4.93 | 3.75 | 1.56 |
| 19:30 | 5963 | NK Celje vs Domzale | 1.80 | 3.45 | 3.76 |
| 20:00 | 2108 | FC Zurich vs FC Luzern | 2.09 | 3.41 | 3.20 |
| 20:00 | 3597 | Salernitana vs Bologna | 3.21 | 3.16 | 2.17 |
| 20:30 | 2367 | Chelsea vs Everton | 1.43 | 4.10 | 6.80 |
| 20:30 | 3648 | Espanyol vs Celta Vigo | 2.74 | 3.09 | 2.49 |
| 20:30 | 4447 | Borussia Dortmund vs FC Koln | 1.43 | 4.49 | 5.99 |
| 20:45 | 2236 | Manchester City vs Burnley | 1.21 | 5.52 | 11.58 |
| 20:45 | 5644 | Emmen vs Sparta Rotterdam | 2.50 | 3.05 | 2.75 |
| 21:00 | 2253 | Maritzburg Utd vs Kaizer Chiefs | 4.13 | 3.08 | 1.91 |
| 21:00 | 2855 | Benfica vs Vitoria Guimaraes | 1.17 | 6.21 | 14.03 |
| 21:00 | 5308 | FC Arouca vs Pacos Ferreira | 2.04 | 3.27 | 3.47 |
| 22:45 | 5453 | Udinese vs AC Milan | 3.19 | 3.24 | 2.14 |
| 23:00 | 3229 | Waalwick vs NEC Nijmegen | 2.41 | 3.29 | 2.70 |
| 23:00 | 3520 | Lens vs Angers | 1.23 | 5.57 | 9.95 |
| 23:00 | 5476 | Atletico Madrid vs Valencia | 1.55 | 3.77 | 5.62 |
| 23:30 | 3560 | GD Estoril vs GD Chaves | 2.12 | 3.16 | 3.37 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# CHAMA ASHIKILIA FUNGUO SIMBA ROBO FAINALI CAF

**Na Hadija Mngwai**

KIUNGO wa kimataifa wa Simba kutoka Zambia, Clatous Chama, amekabidhiwa 'mikoba' ya kuhakikisha timu yake inapata ushindi dhidi ya Horoya AC na kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika yanayoendelea barani hapa.

Simba inatarajia kuwakaribisha Horoya AC kutoka Guinea katika mechi ya Kundi C itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili jana klabu hiyo ina imani kubwa na kikosi chake kitapambana kusaka ushindi na hatimaye kusonga mbele katika mashindano hayo.

Ahmed alisema maandalizi kuelekea mechi hiyo yamekamilika na wanawaomba mashabiki na wanachama kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya kuchagiza ushindi.

Aliongeza ubora wa sasa wa Chama unawaongezea matumaini ya kuivusha timu hiyo kama alivyowahi kufanya katika misimu mingine pale timu ilipokuwa kwenye kipindi kigumu.

"Tulipata ushindi katika mechi kama hii dhidi ya AS Vita (DRC), na tukaingia hatua inayofuata, ile ya Nkana (Zambia), ilikuwa ya hatua ya makundi, na tulifanikiwa kuwatoa, hii ni ya kwenda robo fainali, tulihitaji ushindi na tuliupata, Chama na Shabalala (Mohammed Hussein), wakatupeleka robo fainali.

Na mazingira kama haya yalijitokeza msimu uliopita katika Kombe la Shirikisho tukafanikiwa kuvuka, safari hii kwenye Ligi ya Mabingwa, hivyo tunakwenda kuandika historia Jumamosi," alisema Ahmed.

Aliongeza wachezaji wote wanatambua ili wavuke hatua hii, ni lazima watimize wajibu wao kwa asilimia 100 na hawana mashaka kikosi chao.

"Tuna beki bora Inonga (Henock), na kama haitoshi tuna mchezaji bora wa CAF wa wiki, Chama (mwamba), hivyo hatuna wasiwasi na tunaamini kupitia wao tutafanya vizuri," Ahmed alisema.




# *Simba SC katika dakika 90 hatari*

INATOKA UK 24

wachezaji wangu hasa katika mipira ya kona na faulo, ili kutowapa nafasi wapinzani wetu kupata matokeo," alisema Robertinho.

Nahodha Msaidizi wa Simba, Shomari Kapombe, alisema wamejiandaa vizuri na wako tayari kiakili na kinguvu kupambana kusaka ushindi ili kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Kapombe alisema benchi la ufundi limefanya kazi kubwa na sasa majukumu yamebaki kwao wachezaji kupambana na wanapeperusha vyema bendera ya Taifa na kuendeleza kuitangaza Tanzania zaidi ya walivyofanya misimu iliyopita.

"Mazungumzo yetu tunapokuwa kambini hakuna zaidi ya kutafuta ushindi, tumefanya maandalizi mazuri , mwalimu amemaliza kila kitu katika uwanja wa mazoezi, tumepokea mbinu za kiufundi kutoka kwa benchi la ufundi na tunaenda kusaka pointi tatu dhidi ya Horoya AC," alisema Kapombe.

Naye Kocha Mkuu wa Horoya AC, Sekou Soumaah Diego, alisema timu yake imejiandaa vizuri kwa ajili ya kusaka ushindi dhidi ya Simba licha ya kutambua utakuwa mchezo mgumu na wenye ushindani mkubwa.

Diego alisema amejiandaa kukutana na ushindani kwa sababu watakuwa wanacheza ugenini na hiyo ni hali ya kawaida.

Alongeza hawezi kuweka mbinu zake hadharani ila ataingia na na mfumo tofauti na walivyocheza katika mechi iliyopita ili kujihakikisha kuondoka na alama tatu muhimu.

"Tuko fiti kimwili na kiakili kwa sababu tunafahamu Simba wanapocheza mechi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ni ngumu kupata matokeo, lakini sisi tuko tayari kusaka matokeo mazuri na kuahidi mambo mazuri yataonekana uwanjani," alisema kocha huyo.

Daouda Camara, nahodha wa Horoya AC alisema wamepata maandalizi mazuri na wamekuja Tanzania kutafufa matokeo mazuri na si kutalii. "Tumekuja kutafuta matokeo mazuri, mchezo utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu tunahitaji ushindi na Simba nao wanahitaji kutumia vizuri uwanja wao wa nyumbani. Akili na nguvu zetu zinafikiria kucheza robo fainali," alisema Camara. Wakati huo huo katika kuongeza hamasa, viongozi wa Simba wameahidi kuwapatia wachezaji wap kitita cha Sh. milioni 200 endapo watashinda mechi ya leo.

Katika hatua nyingine, Kundi la Simba HQ linaloongozwa na Mwenyekiti wake, Farough Baghozah, jana jioni lilikabidhi kiasi cha Sh. milioni 10 kwa wachezaji wa timu hiyo ili kuwahamasisha kupambana kupata ushindi.

Baghozah alisema msimu huu wameamua kuja tofauti kwa kukabidhi kwanza fedha kabla ya mchezo na mambo mengine mazuri yatafuata baada ya kumalizika kwa mechi hiyo.

# Michezo

Nipashe

Jumamosi Machi 18, 2023





Odegaard afunguka kufikiria taji la EPL UK. 21




Wachezaji wa Simba kutoka kushoto ni Erasto Nyoni, Pape Sakho, Aishi Manula na Shomary Kapombe wakifanya mazoezi ya mwisho ili kujiandaa kuwavaa Horoya AC kutoka Guinea kwa ajili ya mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba SC katika dakika 90 hatari

**Na Saada Akida**

## ●●● Mnyama anahitaji ushindi ili kumaliza kazi, Sakho aitwa Segenal kwa...

TUNATAKA ushindi, hayo ni maneno yanayotamkwa na kocha, wachezaji, mashabiki na viongozi wa Simba kuelekea mechi ya Kundi C ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Horoya AC itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Simba na Horoya AC kutoka Guinea, kila upande unahitaji ushindi ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano hayo, kabla ya kusubiri mechi moja ya mwisho.**

Katika kujiandaa na mechi hiyo, kikosi cha Wekundu hao wa Msimbazi kilifanya mazoezi yake ya mwisho jana asubuhi wakati wageni, Horoya AC wao walijifua jioni kwenye Uwanja huo wa Benjamin Mkapa.

Simba inashuka dimbani ikiwa na pointi sita mkononi na matokeo ya ushindi yataifanya kufikisha alama tisa ambazo hazitafikiwa na timu nyingine kwenye kundi lao linaloongozwa na Raja Casablanca ambayo tayari imeshatinga robo fainali kutokana na kujikusanyia pointi 12.

Kocha wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' amesema anaingia katika mchezo huo akiwa na mpango mkakati wa kufanya mashambulizi ya mapema ili kusaka ushindi na dhamana hiyo akiwapa washambuliaji wake, Mosses Phiri, Jean Baleke, John Bocco, Kibu Denis na Pape Sakho ambaye jana aliitwa katika kikosi cha Timu ya Taifa ya Senegal kwa mara ya kwanza.

Robertinho alisema amekamilisha kuwaandaa wachezaji wake kiufundi, kimbinu na kuwajenga vizuri kiakili kwa lengo la kumiliki mpira kwa muda mrefu na kuwakabili vyema wapinzani wao Horoya AC yenye nyota warefu na wenye nguvu.

Kocha huyo alisema hatakuwa na mabadiliko makubwa ya kikosi na atatumia pia mbinu za ushindi zilizowasaidia katika mechi zilizopita ambazo walifanikiwa kupata matokeo mazuri.

"Ushirikiano uliopo ndani ya kikosi ni chachu ya ushindi, mashindano haya sio rahisi, anaimani wachezaji wakicheza kitimu watapata matokeo mazuri na ushindi.

Ni kweli Horoya AC ina wachezaji warefu na wenye nguvu, nimewaandaa vizuri

INAENDELEA UK 23

# Yanga Sc yaonyesha ramani ya ushindi

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa US Monastir, Darko Novic, akisema mechi ya kesho itakuwa ngumu zaidi kuliko iliyochezwa nchini Tunisia, Yanga imesema ina sababu tatu muhimu za kushinda mchezo huo wa Kombe la Shirikisho Afrika utakaochezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alitaja sababu ya kwanza ya kupata ushindi dhidi ya US Monastir ni wao wanataka kufuzu tiketi ya kucheza hatua ya robo fainali kabla ya mechi ya mwisho, lakini pia wanahitaji kulipa deni la kufungwa katika mechi ya kwanza iliyochezwa Tunis.

Kamwe alisema pia Yanga imejipanga kutibua rekodi ya timu hiyo ya kutopoteza mechi yoyote kwenye kundi lao.

"Nilitegemea kwa sababu wamefuzu watakuja wachache, lakini wamekuja watu wengi, hadi rais wa klabu, inaonyesha kabisa wamepania, lakini sisi tuko vizuri na wachezaji wetu wamesema wanautaka mchezo, lakini mabao yao lazima yalipwe, yaani lazima tumalizane nao, tatu Monastir anataka kujifanya kama Raja Casablanca ya kutaka kumaliza mechi zake za makundi bila kupoteza, tunataka Dar es Salaam kuwe kwa moto kwake," alisema Kamwe.

Aliongeza wanataka Waarabu hao waione mechi hiyo si rahisi na wafahamu katika kundi lao, watakutana na ushindani kutoka kwa Yanga na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Naye Darko aliliambia gazeti hili hii ni mara ya kwanza kwa timu yao kucheza hatua ya makundi ya michuano hiyo mikubwa na mwanzoni wachezaji wake walicheza na pesha.

"Kwa sasa wameshazoea, japo tumeshafuzu lakini tunacheza kwa nguvu ile ile, ila hatutokuwa na pesha tena, nadhani mechi itakuwa ngumu kuliko hata iliyochezwa Tunisia," alisema kocha huyo wa US Monastir.

Kikosi cha US Monastir kiliwasili nchini alfajiri wa kuamkia jana, kocha wao Mserbia alitabiri mchezo huo utakuwa mgumu zaidi kwa sababu unafanyika kwenye ardhi ya Tanzania.

Aliongeza sasa hivi wachezaji wake hawatacheza kwa pesha sana kwa sababu wameshapata uzoefu na mechi za hatua ya makundi.

Mechi nyingine ya kundi hilo itakuwa ni kati ya AS Real Bamako ya Mali ambayo itawakaribisha TP Mazembe kwenye Uwanja wa 26 Mars ulioko katika jiji la Bamako.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002